# Nipashe

Jumamosi Agosti 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579999

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania

"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on **24th August, 2019,** "Entrance is free". For details **www.alumni.sjuit.ac.tz**

For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505

215359802




## RC azuia likizo za watumishi hadi kilele Mwenge wa Uhuru

UKURASA 4

# Ramaphosa atangaza neema kwa Tanzania

UKURASA 2



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Matamela Ramaphosa (kulia), akiwa na mwenyeji wake, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wakiangalia makaburi ya Wapigania Uhuru wa Afrika Kusini, katika kambi ya Mazimbu, mjini Morogoro jana. **PICHA: OWM**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### IDADI VIFO AJALI YA MAFUTA YAFIKIA 93

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta mkoani Morogoro imeongezeka na kufika 93 baada ya majeruhi wengine wanne...

UKURASA WA 5

### WAZIRI AAGIZA WADAIWA SUGU ARDHI WAKAMATWE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameiagiza idara ya ardhi katika Halmashauri ya Sikonge kuhakikisha inawafikisha kwenye...

## Zitto awapiga chenga polisi

UKURASA 2

## Ma- DED sasa kikaangoni vitambulisho wajasiriamali

UKURASA 4

**MICHEZO** KMC YAJA NA 'TOGETHER WE CAN' KUIUA AS KIGALI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6




# Ramaphosa atangaza neema kwa Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi,**
MOROGORO

AFRIKA Kusini imeendelea kutoa neema kwa Tanzania baada ya jana Rais wake, Cyril Ramaphosa, kuahidi kukifanya kituo cha utalii kilichokuwa kituo cha ukombozi kwa wapigania uhuru wa nchi za kusini mwa Afrika cha Solomon Mahlangu kilichoko katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro.

Vilevile, ameahidi wanafunzi na walimu walioko katika Shule ya Sekondari Chief Albert Luthuli iliyoko kwenye kituo hicho, kushirikiana kielimu na mojawapo ya shule za sekondari za Afrika Kusini kwa lengo la kuendeleza undugu uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Ramaphosa alitangaza neema hiyo jana mkoani Morogoro alipotembelea kituo hicho kilichoko eneo la Mazimbu kilichotumiwa na wanaharakati kudai uhuru na kukomesha vitendo vya ubaguzi wa rangi Afrika Kusini.

"Kuna haja kwa serikali za nchi ya Tanzania na Afrika Kusini kushirikiana kwa pamoja katika kuliendeleza eneo hili, mazao yanayozalishwa katika Mkoa wa Morogoro kuuzwa Afrika Kusini, hivyo hivyo kwa bidhaa za Afrika Kusini kuuzwa Tanzania," Ramaphosa alisema.

Alisema serikali za Tanzania na Afrika Kusini zinapaswa kuhakikisha zinaimarisha miundombinu ya eneo hilo na kutoa ajira kwa wakazi wanaolizunguka.

Rais Ramaphosa alisema Kituo cha Solomon Mahlangu kinaendelea kukumbukwa na wananchi wa Afrika Kusini kwa

INAENDELEA UK. 8




Bendera za nchi wanachama wa SADC, zikipeperuka katika mzunguko wa makutano ya Barabara za Sokoine, Kurasini na Gerezani, eneo la majani ya chai, jijini Dar es Salaam jana huku Jeshi la Polisi likiwa limeimarisha ulinzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Zitto aingia matatani SADC

**Na Mariam Magili**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam jana lilivunja mkutano wa viongozi wa ACT-Wazalendo na waandishi wa habari, huku likiwakamata baadhi ya viongozi wa chama hicho.

Mkutano huo uliokuwa ufanyike jana kuanzia saa tano asubuhi, ulikuwa umeandaliwa na Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, ukiwa na agenda ya kuzungumzia Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Nusu sasa kabla ya mkutano huo kuanza, Nipashe ilishuhudia magari mawili ya polisi yakiingia kwenye ofisi za makao makuu ya chama hicho yaliyoko Kijitonyama jijini dar es salaam yakiwa na askari wenye bunduki.

Magari hayo yalibaki kwenye ofisi hizo kwa takribani robo saa kisha yakaondoka, lakini baadaye moja lilirejea likiwa na askari polisi sita wenye silaha waliomkamata Katibu Mwenezi wa chama hicho, Ado Shaibu.

Kabla ya kutiwa mbarano, Shaibu aliwaomba askari hao aweke mambo sawa ofisini na aliporuhusiwa, alizungumza na waandishi wa habari waliofika kwenye ofisi hizo, akieleza kuwa mkutano huo usingefanyika tena kutokana na polisi kuagiza Zitto afike kituoni kwa ajili ya mahojiano.

Hata hivyo, Shaibu alisema jeshi hilo halikuweka wazi kituo ambacho Mbunge huyo wa Kigoma Mjini anapaswa kwenda kuripoti kwa ajili ya mahojiano hayo.

"(Polisi) wanamtaka Zitto Kabwe ama mimi kwa ajili ya mahojiano, kwa hiyo, nimewaomba kwamba ni lazima niweke mambo sawa ofisini kabla sijaenda polisi," Shaibu alisema.

Aliongeza kuwa polisi walikwenda nyumbani kwa Zitto kwa lengo la kumkamata kwa ajili ya mahojiano.

"Tusiogope, tusitishike, mapambano yanaendelea," Shaibu alisema akiwa nje ya jengo la ofisi za chama hicho kisha akaingia ndani akiwa amefuatana na askari polisi wawili, mmoja akiwa amevaa sare za Jeshi la Polisi na mwingine akiwa amevaa kiraia.

Baada ya takribani dakika 10, watatu hao walitoka ndani ya ofisi hizo na wakapanda kwenye gari la polisi na haikuelezwa kituo cha polisi ambacho kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alikuwa anepelekwa.

Katika ufafanuzi wake kwa waandishi wa habari waliotaka kufahamu sababu za kukamatwa kwa Shaibu jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Mussa Taibu, alisema Jeshi la Polisi halina shida na Katibu Mwenezi huyo wa ACT-Wazalendo bali Zitto.

"Wamemleta hapa (Kituo cha Polisi Oysterbay) nikamuuliza wewe ni nani maana simjui, niliyemhitaji hapa ni Zitto Kabwe, kwa hiyo sisi wala hatuna shida na Shaibu," Kamanda Taibu alisema.

"Mimi sijui kwamba palikuwa na mkutano, labda ninyi ndiyo mniambie, mimi nimemwita Zitto Kabwe kwa ajili ya mahojiano na sasa hivi nimetoka kumpigia, mara ya kwanza hajapokea simu yangu na sasa hivi hapatikani kabisa."

## Ugeni mzito wawasili nchini

**Na Beatrice Moses**

UGENI mzito wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umewasili nchini kuhudhuria mkutano wa 39 wa jumuiya hiyo utakaofanyika jijini Dar es Salaam leo na kesho.

Viongozi hao waliwasili kuanzia Jumatano wakiongozwa na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa huku Barabara ya Nyerere ikifungwa kwa muda jana kutokana na ujio wa viongozi hao.

Wakuu wa nchi za SADC waliowasili jana ni pamoja na Rais wa Zambia, Edgar Lungu, Rais wa Angola, João Lourenço, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Félix Tshisekedi na Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob ambaye ndiye Mwenyekiti wa SADC anayemaliza muda wake.

Baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini, viongozi hao walipokewa na mawaziri wa Tanzania na viongozi mbalimbali wa serikali huku kukiwa na burudani za ngoma zilizotolewa na wasanii mbalimbali uwanjani huko.

Ratiba ya mkutano huo wa SADC inaonyesha Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo, Dk. Stergomena Tax, ataanza kutoa taarifa ya utangulizi na kufuatiwa na hotuba ya kuwakaribisha wageni itakayotolewa na Mwenyekiti mtarajiwa wa SADC, Rais John Magufuli.

Katibu Mtendaji wa Umoja wa Mataifa (UN) anayeshughulikia Kamisheni ya Uchumi Afrika, Dk, Vera Songwe, pia atawasilisha taarifa kwa viongozi hao, akifuatiwa na Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Akinwumi Adesina.

Ratiba hiyo pia inaonyesha kutakuwa na hotuba ya Rais wa DRC Congo, Tshisekedi, Rais wa Madagascar, Andry Rajoelina na Rais wa Comoro, Azali Assoumani.

Mwenyekiti wa SADC, Dk. Geingob, atatoa tuzo kwa washindi wanafunzi wa shule za sekondari bora za kanda kwa kuandika insha kuhusu masuala jumuiya hiyo.

Baada ya kutoa zawadi, Rais Geingob atatoa hotuba yake na kutangaza kuachia ngazi ili kumkaribisha Mwenyekiti mpya wa SADC, Rais Magufuli kisha viongozi hao watakwenda Ikulu jijini .

Katika mkutano huo, mambo kadhaa yanatarajiwa kujadiliwa ikiwa ni pamoja na mapendekezo 107 yaliyotolewa na Baraza la Mawaziri la SADC lililomaliza vikao vyake juzi.

Nchi 16 zinazounda SADC ni Tanzania, Malawi, DRC Congo, Namibia, Angola, Afrika Kusini, Shelisheli, Mauritius, Comoro, Madagascar, Botswana, Eswatini, Zambia, Zimbabwe, Msumbiji na Lesotho.






Meneja wa Jengo la Tatu la Abiria la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Mhandisi Burton Komba (mwenye fimbo) akiwaeleza mambo mbalimbali Mabalozi 42 wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani, walipotembelea jengo hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mabalozi waona fursa uwanja wa ndege Dar

**Na Waandishi Wetu**

MABALOZI wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa 42 duniani, wamesema kukamilika kwa ujenzi wa jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) kutafungua fursa za uchumi nchini.

Wamesema watalii wengi pia watakuja nchini kwa sababu ndege kubwa zitatua, wawekezaji wa viwanda watajitokeza kutokana na kuwapo kwa umeme wa uhakika kupitia mradi wa kufua umeme wa maporomoko ya maji katika Mto Rufiji na miundombinu ya usafiri kama mradi wa reli ya kisasa (SGR).

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam walipotembelea jengo la tatu la uwanja huo, mabalozi hao walisema utatangaza taswira ya Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani hasa wakati huu ambao marais wa nchi 16 watakuwa nchini kushiriki Mkutano wa 39 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Balozi wa Tanzania Ujerumani, Dk. Abdallah Possi, alisema amepata bahati ya kutembelea viwanja vingi duniani na kwa jinsi JNIA ulivyotengenezwa anaamini kutafungua fursa mbalimbali za uwekezaji.

Alisema kazi ya mabalozi ni kutangaza vivutio vilivyopo nchini ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali.

**INAENDELEA UK. 8**

# Watoto wapigania uhuru walilia mafao

**Na Christina Haule,** MOROGORO

UJIO wa Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, nchini Tanzania umeibua mijadala kwa jamaa za waliokuwa wakimbizi katika makazi ya Mzimbu, Kampasi ya Solomon Mahlangu, wakidai kupewa mafao kutokana na vifo vya wazazi wao.

Jamaa hao walisema hayo jana wakati wakizungumza kwenye ujio wa Rais Ramaphosa kwenye kambi ya Solomon Mahlangu Mazimbu mkoani hapa. Miongoni mwa jamaa hao ni watoto walioachwa na wazazi wao (baba) waliondoka baada ya kurejea kwao mwaka 1992 na kubaki nchini huku wazazi wao wa kike pekee wakiendelea kuwahudumia.

Mmoja wa watoto walioachwa na baba yake, Omuto Elias Omathe (21), alisema hajawahi kumwona baba yake licha ya kwamba mama yake alishawahi kumwambia kuwa ameshafariki dunia akiwa Afrika Kusini.

Binti huyo ambaye hakuvumilia na kuamua kumwita Rais Ramaphosa alipokuwa akiondoka kutoka kwenye eneo la makaburi ya wapigania uhuru hao na kuangua kilio akimwomba Rais huyo kuwasaidia watoto kama yeye kupata fursa mbalimbali sambamba na wengine kuwajua wazazi wao kwakuwa waliondoka wakiwa wadogo.

Alisema wako wengi wanaoishi Tanzania na wamekosa fursa mbalimbali ambazo wenzao wanazipata zikiwamo elimu na makazi bora na kuwafanya kujiona kama hawana ndugu.

Omathe aliiomba serikali ya Afrika Kusini kuwawezesha kupata mafao kutokana na baba yake alikuwa mpigania uhuru ambaye aliondoka na kurejea nchini humo na kumwacha akiwa mdogo. Alisema wakipewa mafao kama vile wanavyopewa wengine ambao baba zao wamefariki dunia wakiwa wapigania uhuru nchini humo na serikali inaendelea kuwahudumia, itawasaidia kujikimu katika mahitaji mbalimbali.

Naye mama wa binti huyo, Monica Omathe, alisema amefanya kazi za ndani katika kampasi hiyo muda mrefu tangu mwaka 1981 na kwamba alikutana na baba huyo na kukaa naye lakini baada ya mzazi mwenzie kuondoka, walihamishwa kwenye kambi walizokuwa wanakaa.

# Tanzania, Afrika Kusini kushirikiana maendeleo viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amesema serikali ya Tanzania iko tayari kushirikiana na Afrika Kusini katika kutimiza azma yake ya kukuza uchumi na kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo 2025.

Amesema Tanzania inahitaji uungwaji mkono na serikali ya Afrika Kusini hususan katika kipindi hiki ambacho imedhamiria kuimarisha shughuli za uzalishaji kupitia viwanda.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa ziara ya kiserikali ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), kampasi ya Mazimbu mjini Morogoro.

Majaliwa alisema changamoto zinazoikabili Tanzania katika nyanja mbalimbali zinafanana kwa kiasi fulani na zile za Afrika Kusini kwa kuwa historia za nchi hiyo na jiografia vinafanana na Tanzania.

Kuhusu Mazimbu, Waziri Mkuu alisema lina uhusiano mkubwa na historia ya nchi hizo mbili kwa sababu mtu hawezi kuulezea vizuri uhusiano

**INAENDELEA UK. 8**

SALAMU ZA PONGEZI



MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA **KAMPUNI ZA IPP** WANATOA PONGEZI ZA DHATI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA **DR. JOHN POMBE MAGUFULI** KWA KUCHAGULIWA KUWA MWENYEKITI WA SADC

**HONGERA SANA MHESHIMIWA RAIS**

The Guardian Nipashe

# Idadi vifo ajali ya mafuta yafika 93

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta mkoani Morogoro imeongezeka na kufika 93 baada ya majeruhi wengine wanne waliokuwa wamelazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kufariki dunia jana.

Kufuatia vifo hivyo, idadi ya wagonjwa waliobaki katika hospitali hiyo kubwa zaidi nchini ni 25 kati ya 46 waliokuwa wamefikishwa kupatiwa matibabu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alitoa taarifa hizo jana alipozungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kutembelea hospitali hiyo kuona majeruhi hao.

Alisema wagonjwa wengine 21 wanaoendelea kupatiwa matibabu Muhimbili wamewekwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU).

Alisema madaktari wanafanya kila jitihada kuokoa maisha ya wagonjwa waliobaki ili wapone na kuendelea na shughuli zao za kila siku.

Ummy alisema ili kuhakikisha wagonjwa hao wanapata huduma bora, kila mgonjwa ana nesi wake anayemtazama kwa karibu.

Waziri huyo pia aliagiza kuanzishwa kwa kitengo maalum cha kuhudumia wagonjwa wanaotokana na ajali za moto kitakachokuwa na chumba cha wagonjwa mahututi.

Alisema kuwapo kwa kitengo hicho kutasaidia wagonjwa wanaopata ajali za moto kupata huduma za matibabu kwa wakati na haraka.

Mkuu wa Kitengo cha Dharura cha MNH, Dk. Charles Majinge, alisema wagonjwa wanapewa huduma inayotakiwa na wote waliobaki wamewekwa ICU.

Alisema wagonjwa hao wamewekwa ICU ili kuongeza umakini wa juu zaidi katika kuwahudumia.

Idadi hiyo ya waliopoteza maisha inatokana na ajali ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka eneo la Msamvu mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, akipanda katika gari ya Polisi, baada ya kukamatwa akiwa katika makao makuu ya chama hicho Kijitonyama jijini Dar es Salaam jana, alipokuwa akifanya maandalizi ya mkutano wa waandishi wa habari na kiongozi mkuu wa chama hicho Zitto Kabwe, uliozuiliwa na jeshi hilo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**






# Ma-DED kikaangoni vitambulisho wajasiriamali

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, amewataka wakurugenzi wa halmashauri za manispaa na wilaya mkoani mwake kukamilisha uuzaji wa vitambulisho vya wajasiriamali ndani ya mwezi mmoja kuanzia juzi.

Kiongozi huyo wa mkoa alitoa agizo hilo juzi katika kikao kazi cha watumishi wa halmashauri kilichofanyika kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

Zambi alisema amelazimika kutoa muda huo kutokana na kusuasua kwa uuzwaji wa vitambulisho hivyo. Mkoa wa Lindi ulipatiwa vitambulisho 65,000.

Alisema hajaridhishwa na mwenendo wa uuzwaji wa vitambulisho hivyo ikizingatiwa uuzaji wake ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli.

Alisema mtendaji yeyote kuanzia ngazi ya mtaa, kijiji, kata, tarafa hadi wilaya atakayeshindwa kukamilisha uuzwaji wa vitambulisho hivyo kwa muda wa mwezi mmoja alioutoa, ni vema akajiondoa na kupisha walio na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Alisema ameshangazwa kuona mtumishi anapewa vitambulisho 300 lakini anauza 52, jambo alilodai ni uzembe.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, akizungumza katika kikao hicho, alimhakikishia Zambia kuwa vitambulisho vilivyobaki wilayani mwake vitakuwa vimeshauzwa kufikia mwishoni mwa mwezi huu.

Vitambulisho vilivyotengenezwa na Ofisi ya Rais vinauzwa kwa wajasirimali wadogo (mapato ghafi ya chini ya Sh. milioni nne kwa mwaka) kwa bei ya Sh. 20,000 kwa kila kitambulisho.

# RC azuia likizo watumishi siku 90

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, amezuia watumishi wa serikali kwenda likizo kwa muda wa miezi mitatu ili kusimamia miradi ya maendeleo na vitambulisho vya wajasiriamali kwenye maeneo yao na maandalizi ya mapokezi na uzimaji wa Mwenge wa Uhuru.

Zambi alitangaza hatua hiyo juzi alipozungumza katika kikao kazi na watumishi mbalimbali wakiwamo maofisa tarafa na watendaji wa kata wa halmashauri za wilaya na manispaa ya Lindi kilichofanyika Uwanja wa Ilulu mjini hapa.

Alisema amechukuwa uamuzi huo kutokana na shughuli nyingi zinazoukabili mkoa huo mwaka huu kama vile uzimaji Mwenge wa Uhuru Oktoba 14, mwaka huu.

Zambi alisema kutokana na majukumu hayo, amelazimika kuzuia watumishi wote wa serikali wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi, watendaji wa halmashauri za wilaya na manispaa, maofisa tarafa, watendaji wa kata, vijiji, mitaa na vitongoji kutoenda likizo kwa kipindi hicho cha miezi mitatu.

"Kuanzia leo (juzi), nazuia likizo zote za watumishi wote wa serikali hadi Desemba mwaka huu," Zambi alitangaza.

Alisema mkoa una miradi mingi kama vile ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na shule lakini kutokana na kukosa usimamizi wa karibu utekelezaji wake umekuwa ukilegalega.

## HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza wadaiwa sugu ardhi wakamatwe

**Na Mwandishi Wetu,**
SIKONGE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameiagiza idara ya ardhi katika Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora kuhakikisha inawafikisha kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi wa wilaya hiyo wanaodaiwa takriban Sh. milioni 150.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi katika ziara yake ya kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya ardhi na kukagua masjala ya ardhi na mifumo ya ukusanyaji kodi kwa njia ya kielektroniki mkoani Tabora.

Dk. Mabula alieleza kushangazwa na idara ya ardhi katika halmashauri hiyo kushindwa kuwafikisha wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba wakati sheria inaelekeza baada ya siku 14 mdaiwa asipotii wito, afikishwe katika baraza hilo.

Alibainisha kuwa katika Halmashauri ya Sikonge kuna baadhi ya wamiliki wa ardhi ambao kwa mara ya mwisho walilipa kodi ya ardhi mwaka 2000, lakini idara ya ardhi imeshindwa kuwadai ama kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Kaimu Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Martin Ukongo, alisema ofisi yake tayari ilishasambaza ilani 105 kwa wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo wa mwaka huu lakini baadhi yao hawajafikishwa kwenye Baraza la Ardhi.

Dk. Mabula pia aliiagiza halmashauri hiyo kupitia idara ya ardhi kuhakikisha inapima mashamba yote yaliyoko katika halmashauri hiyo, akibainisha kuwa kutopimwa kwa mashamba hayo kunatoa fursa kwa wamiliki wake kutolipa kodi ya ardhi.

"Sikonge mna mashamba hayajapimwa wakati ni ya wafanyabiashara wakubwa, hapa wanakwepa kulipa kodi, 'why' (kwanini) hamjawapimia na kuwapatia hati ili walipe kodi?" Dk. Mabula alihoji.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, alisema wizara sasa imeimarisha mfumo wa ukusanyaji kodi ya pango la ardhi kwa kurahisisha ukadiriaji na kufanya malipo kupitia simu ya mkononi.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri, alimweleza Dk. Mabula kuwa katika mwaka uliopita, wilaya yake ilifanikiwa kukusanya kodi ya pango la ardhi Sh. milioni 29.127, sawa na asilimia 87.55 ya lengo la kukusanya Sh. milioni 33.2.

Magiri alisema wilaya yake imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kama vile kutoa matangazo na kuelimisha jamii kupitia mikutano.

Mbunge wa Sikonge, Joseph Kakunda (CCM), alimpongeza Dk. Mabula kwa kufanya ziara katika wilaya hiyo, akibainisha kuwa amekuwa kiongozi wa kwanza wa wizara hiyo kuitembelea wilaya hiyo toka ianzishwe.

Kakunda alisema wilaya hiyo iko nyuma katika Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na kuomba wizara kuipa kipaumbele katika upimaji ili kuepusha migogoro ya ardhi hasa ile ya wakulima na wafugaji.




Kaimu Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Witonde Fillipo (kulia), akikabidhi moja ya mashine mbili za kuhifadhi watoto wanaozaliwa kabla ya muda wake (Njiti), yenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, kwa ajili ya kusaidia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo, jana. Wa (pili kulia) ni Meneja wa Bandari Mkoa wa Tanga, Ajuae Mse. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Polisi wanaowakwaza watalii kushughulikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaendelea kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya utalii ikiwamo ya polisi kusimamisha magari yenye watalii mara kwa mara. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, aliyasema hayo juzi alipozungumza na wadau wa utalii nchini katika kongamano la utalii lililofanyika mkoani Arusha.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa utalii nchini imejenga vituo vya ukaguzi wa magari ya utalii ili kupunguza usumbufu kwa watalii barabarani.

Alisema vituo hivyo vitashughulikia masuala ya msingi ikiwa ni pamona na suala madereva wa magari yanayobeba watalii kupimwa kilevi.

Alisema mbali na kilevi, vituo hivyo vitashughulikia vitendo vyote ya uhalifu watakavyofanyiwa watalii.

Kanyasu alisema lengo la serikali ni kupunguza kero kwa watalii ili nchi ifikie lengo la kupata watalii milioni mbili mwaka huu.

Alisema licha ya kujengwa vituo hivyo vya ukaguzi, bado kuna kero ambazo zinafanyiwa kazi lengo ili kuboresha sekta ya utalii nchini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, aliwataka wadau wa utalii kufuata sheria, huku akitoa rai kupewa taarifa za polisi wanaowakwaza watalii. "Nipigieni simu hata saa nane za usiku kwa askari wanawaomba rushwa nishughulike nao," Shana alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema lengo la Arusha kuanzisha vituo vya ukaguzi magari ni kupunguza kero. Alisema wanaamini uwapo wa vituo hivyo utafanya mazingira bora kwa watalii na wafanyabiashara.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasafirishaji Watalii (Tato), Wilbard Chambulo, alisema ujenzi wa vituo hivyo ni hatua muhimu kuwahakikishia watalii usalama wao pindi wakiwa barabani.

Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, alisema Mkoa wa Arusha ni mfano wa kuigwa kwa mikoa mingine kwa kujenga vituo hivyo.

# Ole Nasha akoshwa na miradi Manonga

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, ameeleza kuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya sekta ya elimu katika Jimbo la Manonga wilayani Igunga mkoani Tabora.

Akiwa ziarani wilayani humo juzi, Ole Nasha alitembelea Shule ya Sekondari Ziba na kuipongeza Bodi ya Shule hiyo kwa usimamizi mzuri wa mradi wa ujenzi wa mabweni, madarasa na bwalo la chakula.

Katika mradi huo, Sh. milioni 225 zimtumika kujenga mabweni matatu huku Sh. milioni 40 zikitumika kujenga madarasa mawili.

Ole Nasha aliahidi kutuma timu ya wataalamu kutoka wizarani kwenda kujifunza namna bodi ya shule hiyo ilivyofanikisha ujenzi huo kwa ufanisi wa hali ya juu.

"Maeneo mengi niliyotembelea, fedha zimetumika vibaya na wahusika kutumia zaidi nguvu za wananchi kukamilisha miradi, lakini hawa wametumia fedha zilezile kwa kila kitu na bado kuna Sh. milioni 49 kwenye akaunti. Malizieni kazi iliyobaki maana mkichelewa kuna hatari ya kupanda kwa bei ya vifaa," alisema.

Katika ziara yake hiyo, Ole Nasha pia ametembea Shule Shikizi ya Igumila iliyoko Ziba ambayo serikali imetenga Sh. milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne.

Naibu waziri huyo pia alitembelea Shule ya Sekondari Choma alikokagua mradi wa ujenzi wa mabweni na kuahidi kuwa kama watamaliza mapema, wizara yake itawapa Sh. milioni 100 ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula.

Ole Nasha pia alisema wizara yake inatarajia kutoa Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula katika Shule ya Sekondari Mwisi.

Kiongozi huyo wa serikali pia alisema wizara yake inatarajia kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya uendelezaji wa Veta Manonga na kwamba fedha hizo zitatolewa mara tu baada ya uongozi wa halmashauri kukabidhi hati ya eneo kilipo chuo hicho. Mradi huo ulianzishwa na Shirika la World Vision.

Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), alimshukuru Ole Nasha kwa kutembelea jimbo hilo na kumweleza kuwa wananchi wanaishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuwapatia fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Azam tunataka soka la kiungwana mkimulika Caf

**MABINGWA** wa Ligi Kuu Bara, Simba na washindi wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini (FA Cup), Azam FC, leo watashuka dimbani kuwania Ngao ya Jamii katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Taifa majira ya saa moja usiku.

Kupigwa kwa mechi hiyo ni ishara ya kufunguliwa kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2019/20, unaotarajiwa kuanza mwishoni mwa wiki ijayo katika viwanja mbalimbali hapa nchini. Tayari makocha wote wawili wa timu hizo, Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems na wa Azam FC, Mrundi Etienne Ndayiragije, kila mmoja amejinasibu kufanya vizuri katika mechi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na upinzani mkali huku wakiutumia kujiandaa kuelekea mechi zao za kimataifa za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba itashuka dimbani ikitoka kulazimisha sare tasa ugenini Msumbiji dhidi ya UD Songo kwenye mechi ya hatua ya awali ya Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC ikishuka uwanjani ikiwa na maumivu ya kipigo cha bao 1-0 ilichokipata nchini Ethiopia dhidi ya Fasil Kenema katika mchezo wa raundi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika. Hata hivyo, morali kwa Azam FC unaweza kuongezeka kutokana juzi kuichapa Namungo FC mabao 8-1, kwenye mechi ya kirafiki.

Hivyo, mashabiki wa timu hizo na wadau wa soka nchini kama ilivyo kwa Nipashe wanatarajia kushuhudia kandanda safi na la kuvutia, lakini pia wakitumia mchezo huo kuweka matarajio yao ya kuziona timu hizo zikishinda mechi zao za marudiano za kimataifa mwishoni mwa wiki ijayo.

Tunatarajia pia kuona waamuzi wakitenda haki kwa kufuata sheria 17 za soka na kutokuwapo kwa timu moja kubebwa katika mchezo huo ambao utakuwa wa kwanza kwa Kocha Ndayiragije kuingoza Azam FC baada ya kujiunga nayo akitoka kuinoa KMC FC msimu uliopita. Aidha, kwa upande wa wachezaji tunatamani kuona wakionyesha kandanda safi na kutocheza kwa kukamiana na rafu zisizo za msingi kwani kwa kufanya hivyo, wanaweza kujikuta wakisababishiana majeraha yasiyo ya lazima jambo litakalozigharimu timu zao kwenye mechi zao za marudiano za kimataifa wiki ijayo.


Tunataka kuona wachezaji wa pande zote wakifurahia soka lao kwa kucheza kwa kuheshimiana kwa kila mmoja kufikiria zaidi michuano iliyo mbele yao ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika. Ingawa upinzani hauwezi kuzuilika huku kila timu ikihitaji kufungua msimu kwa kutwaa taji la kwanza, lakini wachezaji wanapaswa kutanguliza mbele utu wao wa kuona kila mmoja anamaliza mechi hiyo salama pasipo kupata majeraha yanayoweza kumfanya kukosa mchezo ujao wa michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

Lengo letu si kuziona Simba na Azam pekee zikisonga mbele katika michuano hiyo ya Caf, bali tunatamani pia kuiona Yanga ikipeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa na KMC inayobeba jukumu hilo upande wa Kombe la Shirikisho, zikifanya vizuri na kusonga mbele, ndiyo maana tunasisitiza katika mechi hiyo ya Ngao ya Jamii wachezaji kuona wajibu huo kwa kucheza kistarabu zaidi.

Kadhalika, mashabiki wa soka hawana budi kujitokeza kwa wingi uwanjani kuzishangilia timu zao huku Jeshi la Polisi likichukua nafasi yake ipasavyo katika kuhakikisha amani inatawala kwenye mechi hiyo itakayopigwa leo usiku.

Tunataka kuona amani ikiendelea kutawala katika viwanja vyetu vya soka kuanzia uwanjani kwa wachezaji hadi majukwaani kwa mashabiki, hivyo jukumu la ulinzi halipaswi kuwa la Jeshi la Polisi pekee, bali kila mmoja hana budi kuwa mlinzi wa mwenzake, na hilo likitekelezeka tutaendelea kufurahia soka letu bila bughudha yoyote kwa msimu mzima. Tunazitakia kila la heri Simba na Azam huku zikitanguliza kucheza kiungwana zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Simba, Yanga maneno makali hayavunji mfupa

**MANENO** tu hayawezi kuvunja mifupa hata yakawa makali kiasi gani. Methali hii hutumiwa na mtu anayepuuza maneno yaliyosemwa na mtu mwingine na ambayo hayawezi kumdhuru kwa namna yoyote au hayamzuii kutekeleza atakalo.

Hakuna mpiganaji anayekwenda kupambana akisema atashindwa. Lazima atoe maneno ya vitisho dhidi ya mpinzani wake ili kumwogopesha na kumkatisha tamaa.

Jambo hili lanikumbusha vita vya (si vita 'ya') Kagera. Aliyekuwa Rais wa Uganda, Jenerali Idi Amin 'Dada' (Mungu amrehemu) alijitapa sana kuwa ndege zake za kivita zingeweza kulishambulia jiji la Dar es Salaam na kurejea Uganda katika muda wa dakika tano!

Aliyekuwa Rais wa Tanzania wakati ule, Mwalimu Julius Nyerere (Mungu amrehemu), hakutaka vita bali alipenda mapatano ingawa askari wa jeshi la Uganda walikwisha ingia mkoani Kagera nchini Tanzania kwa madai kuwa ni 'eneo la Uganda!'

Vitisho vya Idi Amin 'Dada' wakati askari wake wakiwa tayari wameingia Tanzania kupitia Kagera na kuharibu daraja linalozitenganisha Uganda na Tanzania, vilimlazimu Mwalimu Nyerere aamuru majeshi ya Tanzania kwenda kukomboa ardhi ya Tanzania iliyokaliwa na wavamizi.

Mwalimu Nyerere alisema: "Tutampiga Idi Amin. Sababu tunazo, nia tunayo na uwezo tunao." Kuanzia hapo askari wakakamavu wa Tanzania wakaingia vitani, wakawafurusha (fukuza watu au wanyama) wanajeshi wa Uganda, kuwaua na kuteka baadhi ya vifaa vyao vya vita walivyoviacha nyuma kukimbia mashambulizi.

Hata wanajeshi wa Libya waliopelekwa Uganda kuisaidia, hawakufua dafu kwa majeshi ya Tanzania. Aliyekuwa kiongozi wa Libya ambaye sasa ni marehemu, alimwomba Rais Nyerere awaachie askari wake na angekuwa tayari kuipa Tanzania fungu kubwa la hela. Mwalimu Nyerere alikataa akisema hafanyi biashara ya kuuza binadamu; akawaachia bila malipo, wakarejea kwao.

Jenerali Idi Amin 'Dada' alikimbia baada ya kusikia wanajeshi wa Tanzania wameingia Uganda. Akaikimbia nchi yake na kusahau bastola yake chumbani! Alifia ughaibuni kwa Waarabu.

Wahenga walisema: "Mwenye kelele hana neno." Aghalabu mtu anayepiga kelele huwa hana madhara yoyote. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa hatupaswi kumwogopa mtu mwenye kelele au fujo kwani kwa kawaida hana neno.

Pia ilisemwa kuwa "Msi hadhari hujifunga kwa ulimi wake." Asiyetahadhari katika usemaji wake huenda akajitosa taabani kutokana na asemayo. Methali hii yatunasihi tusiwe na tabia ya kupayukapayuka bila ya kuyazingatia, kuyapima na kuyatathmini tuyasemayo hasa katika kadamnasi (hadharani; jahara).

Kuna wakati timu za Simba na Yanga huponzwa na sifa za magazeti yetu ya michezo. Umwambiapo mwenzako 'nitakupiga,' kwa mtu jasiri maana yake unamwambia ajiandae kwa vita.

Wakati wewe uliyemtahadharisha mpinzani wako, unapoingia vitani kwa mbwembwe, mpinzani wako ataingia kwa tahadhari na nguvu na hatimaye kukushangaza. Unaposhangaa, yeye atajitahidi kukupiga na ikishindakana, wote mtarudi nyuma kama majogoo wanaoogopana!

Michezo ya hivi karibuni ya kimataifa, Simba ilipambana ugenini dhidi ya UD do Songo ya Msumbiji na matokeo kuwa suluhu ya kutofungana. Yanga ilikuwa nyumbani kupimana ubavu na Township Rollers ya Botswana na kufungana 1-1 Yanga ikisawazisha kwa penalti, wakati Azam ikiwa ugenini Ethiopia ikipoteza mchezo kwa kufungwa na timu ya Fasil Kenema bao 1-0 na KMC ikitoka suluhu ugenini Rwanda dhidi ya AS Kigali.

Nathubutu kusema suluhu, sare na kushindwa kwa timu nilizozitaja kumesababishwa na sifa za magazeti ya michezo nchini. Badala ya kuzihimiza timu hizo kucheza kwa tahadhari na bidii, yalizisifu mno na kuwavimbisha vichwa baadhi ya wachezaji kuwa hakuna timu za kuwashinda! Hakuna timu inayocheza ili ishindwe kwani kila moja ina nia ya ushindi.

Sasa soma vichwa vya habari za magazeti ya michezo: "Mtakoma! Simba mpya ni krosi, kona, bao." "HAMTAAMINI Jeshi tayari kwa vita, MO apewa jeuri mpya." "MO Banka, Sibomana mtapata tabu sana." Vichwa vya habari kama hivi ndivyo vinavyowaponza wachezaji wetu wakiamini kushinda tu kana kwamba wapinzani wao hawataki ushindi!

Unapomtisha mpinzani wako kwa maneno kwa utampiga, maana yake ni kumzindua ajiandae kupigwa. Hivyo hujiandaa hasa kwa lengo na nia ya kukushinda wewe unayetamba kumpiga.

Nadhani ni bora magazeti yetu yawahimize wachezaji wa timu zetu kufanya mazoezi magumu na kuwa na mbinu (si ushirikina wala rushwa) za kisasa ili kuzishinda timu ngeni. Wanachama na mashabiki hupata wakati mgumu sana timu zao zinaposhindwa nje ya nchi na wakati mwingine hata nyumbani! Matokeo yake ni idadi ya wanaokwenda uwanjani kuzishangilia timu zao kupungua hivyo timu huathirika kimapato.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI KITAIFA

# Jela miaka 30 kumpa ujauzito mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma, imemhukumu mkazi wa Mwanga Majengo Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Isack Balayabala (25), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumpatia ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Kaulananga.

Hukumu hiyo iletolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Elia Baha, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasina shaka yoyote.

Hakimu Baha alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na vijana wengine wenye tabia ya uharibifu kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi watano na kielelezo kimoja ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alimpa ujauzito mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa).

Baha alisema upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasina shaka kwa sababu mwanafunzi mwenyewe alithibitisha kuwa aliyempa ujauzito ni mshtakiwa huyo. Pia baba wa mwanafunzi huyo naye alithibitisha kuwa aliyempa ujauzito mtoto wake ni mshtakiwa.

Alisema mshtakiwa huyo baada ya mwanafunzi kumwambia kuwa ana ujauzito wake, alimchukua na kumpeleka nyumba za kulala wageni za Mlole, Katubuka na Nazareth kisha kumpangia chumba Masanga.

Hata hivyo, baada ya kumpangia chumba, mshtakiwa alimtelekeza mwanafunzi huyo na kuamua kurudi nyumbani kwa wazazi wake.

Aidha, alisema baada ya mwanafunzi huyo kurudi kwa wazazi wake, walimchukua na kumpeleka Kituo Kikuu cha Polisi na kupewa fomu ya matibabu (PF3) kisha kupelekwa katika Hosptali ya Rufani ya Mkoa ya Maweni na alipofanyiwa uchunguzi, daktari alibaini ana mimba ya wiki 11.

Hakimu alisema baada ya kubaini kuwa mwanafunzi huyo ana ujauzito, wazazi walimbana mwanafunzi na kumtaja kuwa aliyempa hiyo mimba ni mshtakiwa ndipo alitafutwa na kukamatwa na baada ya mahojiano alifikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Katika kutoa hukumu, Hakimu Baha alisema ameangalia ushahidi wa pande zote mbili na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama hiyo inamtia hatiani mshtakiwa kwa kosa aliloshtakiwa nalo. Kabla ya kutoa adhabu, mahakama hiyo ilimtaka mshtakiwa ajitetee ili kumpunguzia adhabu na kusema: "Naomba mahakama hii isitoe adhabu kali kwa sababu nimesingiziwa."

Hakimu Baha alitupilia mbali utetezi huo wa mshtakiwa na kusema: "Mahakama hii imeangalia mambo matatu ambayo ni ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka umejitosheleza, matakwa ya sheria na utetezi wa mshtakiwa huyo.

# Wapongeza majukumu kurejeshwa TBS

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

WAFANYABIASHARA wameunga mkono hatua ya serikali kurejesha kwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) baadhi ya majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na iliyokuwa Mamlaka ya Dawa na Chakula Tanzania (TFDA).

Wamesema hatua hiyo imeondoa changamoto mbalimbali walizokuwa wakikabiliana nazo.

Kauli hiyo ilitolewa na wafanyabiashara hao kwa nyakati tofauti walipozungumza na gazeti hili jana pamoja na jinsi walivyofaidika na elimu iliyotolewa na TBS kwenye Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) yaliyomalizika hivi karibuni kwenye viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Paul John, alisema uamuzi wa serikali kwa bidhaa za chakula na vipodozi kushughulikiwa na TBS sasa unarahisisha utaratibu wa kupata alama ya ubora ya TBS.

Naye Edna Edward alisema: "Kwa sasa tunashuruku utaratibu huu umerahisisha maombi ya kupata alama ya ubora. Leo hii muombaji anatuma maombi yake TBS na shirika lifanye pia ukaguzi wa majengo na hii imepunguza changamoto tulizokuwa tunakutana nazo," alisema.

Ofisa Masoko TBS, Rhoda Mayugu, alisema walishiriki maonyesho haya kama wadau ili kutoa elimu kwa wazalishaji juu ya masuala mbalimbali yahusuyo viwango.

"Vile vile tumefafanua kwa wananchi kuhusu majukumu mapya tulioongezewa baada ya TFDA kubadilishwa majukumu yake pamoja na kuwafahamisha fursa ya huduma bure kwa wajasiriamali wadogo. Hii ni fursa muhimu ambayo inalenga kumwinua mzalishaji aweze kushindana na kuuza bidhaa zake ndani na nje ya nchi bila wasiwasi,"alisema Mayugu.

Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Yekonia Sanga, alitoa wito kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kujitokeza kwa wingi kuthibitisha bure ubora wa bidhaa zao.

"Shirika kwa kushirikiana na Serikali bado linaendelea kuthibitisha ubora wa bidhaa bure kwa muda wa miaka mitatu kama ilivyokuwa awali. Mjasiriamali atapata barua ya utambulisho kutoka SIDO itakayomuwezesha kuthibitishiwa bidhaa zake bure," alisema Sanga. Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, alitoa mwito kwa wakulima wanaosindika mazao yao wafike TBS ili kuthibitishiwa ubora wa bidhaa zao.

Ili kufanikisha suala hilo, Pinda alitaka TBS kupunguza urasimu unaoweza kuwa kikwazo katika kuwahudumia wajasiriamali.

"Nimepita kwenye mabanda yenu na nimefurahishwa na hatua mliofikia ya kusindika mazao ya vyakula na kuongeza thamani, vifungashio mnavyotumia ni vizuri sana na bidhaa zenu zinaweza kuuzika hadi nje ya mipaka kanda yenu na nje ya nchi ila mmepungukiwa na kitu kimoja tu alama ya ubora ya TBS ili kufanikisha hilo," alisema Pinda na kuongeza:

"TBS pia nawaomba msiwe na urasimu katika kuwasaidia hawa wajasiriamali wadogo na wakati kupata alama ya ubora ya TBS ili kuendana adhima ya Rais wa awamu ya tano ya kujenga Tanzania ya viwanda."


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA KUU-DAR ES SALAAM**
**MISC. CIVIL CAUSE NO. 19 OF 2019**

1. MUSSA YUSUF KUNDECHA...............MWOMBAJI
2. ALLY KASSIM MLANZI.......................MWOMBAJI

DHIDI YA

1. EXECUTIVE OFFICER REGISTRATION INSOLVENCY AND TRUSTEESHIP AGENCY
2. THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA ISLAMIC CENTRE
3. ALYASA MTUMWA MAQSOUD
4. MUHIDIN AHAMAD NDOLANGA
5. IDD ZUBERI
6. MSHINDO MAULID NGATANGA
7. MRISHO SHABANI SAID
8. MAHMOUD NASSIR FUNDI
9. OMAR SHABAN GEMBE
10. AHMAD SHABAN MBEGU
11. KHAMIS SALUM KHAMIS
12. ALLU RADHID SHAALY.....................WAJIBU MAOMBI

KWA:
Mohamed Nassir Fundi
Omar Salum Gembe
Dar es salaam

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa waombaji waliotajwa hapo juu, wameleta shauri la maombi ya Madai dhidi yenu: Maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinapatikana katika Mahakama hii, Hivyo basi mnahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii kupitia Wakili au Mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe 9/9/2019 saa tatu (3.00) kamili asubuhi mbele ya Mhe. Jaji B.S Masoud kujibu maombi hayo dhidi yako.

Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnatarajia kuvitumia kwa ajili ya utetezi siku hiyo.

**ANGALIA:**
Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakam ikithibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kitwa shaurini , basi shauri hili linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakam hii leo 9 Agosti,2019

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU - DAR ES SALAAM

115377302



**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) - TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) - TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501



# Wanaume wapewa somo la tiba

**Na Romana Mallya**

WANAUME wameshauriwa kutumia vidonge vya Folic Acid mara kwa mara ili kuePuka uwezekano wa kuzaa watoto wenye matatizo ya mgongo wazi na vichwa vikubwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Mary Ochieng, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam, baada ya kupokea msaada wa mashuka, pampasi na vitu vya kula kutoka First Supermarket kwa ajili ya watoto wenye matatizo hayo waliolazwa MOI.

Ochieng lisema idadi ya watoto wenye matatizo hayo ni kubwa na kila siku wamekuwa wakiwapokea kwenye taasisi hiyo wakitokea mikoa mbalimbali nchini.

"Wito wetu ili tatizo hili lisiendelee nchini, tunawaomba wanaume wawasaidie wake zao watumie dawa za Folic Acid ambazo ndizo zinazosaidia kutozaliwa watoto wenye matatizo ya mgongo wazi na vichwa vikubwa. Mwanaume akitumia na mwanamke alipata ujauzito naye akitumia, hakuna mtoto mwenye mgongo wazi au kichwa kikubwa ambaye atazaliwa," alisema.

Pia alisema tatizo lingine lilipo ni wanaume wengi kuwakimbia wake zao baada ya kuzaliwa watoto wenye matatizo hayo.

"Hapa wodini asilimia kubwa wanawake wamekimbiwa na waume zao baada ya watoto kuzaliwa na matatizo haya. Ili kuzuia huu ulemavu mama anatakiwa kutumia vidonge vya Folic Acid miezi mitatu kabla ya kubeba ujauzito na atumie kila siku mpaka atakapojifungua, folic Acid inatokana na matunda na mbogamboga yenye rangi ya njano na kijani," alisema.

Mary alitoa wito kwa makundi mbalimbali kwenye jamii wajitokeze kusaidia wazazi wenye watoto waliolazwa hapo kwa sababu wanauhitaji mkubwa wa vitu mbalimbali.

Mkurugenzi wa First Supermarket, Devota Mkwawa, alisema ameamua kutoa msaada wa mashuka na pampers na vitu vya kula kwa sababu ni sehemu ya uhitaji wa watoto hao.

"Ninawaahidi wanawake wenzangu, nitarudi tena kwa ajili ya kuwaletea kadi za bima ya afya kwa ajili ya watoto wenu, nimeona nitangulize kwanza msaada huu wakati kadi zikiendelea kushughulikiwa," alisema.

Akitoa neno la shukrani, mama mwenye mtoto mwenye kichwa kikubwa Joyce Tambwe, alisema msaada huo ni mkubwa kwao kwa sababu watoto wao bado ni wadogo wanahitaji pampers na wao muda mwingi wamekuwa wakikaa nao bila kufanya shughuli nyingine za kujiingizia kipato.



Kijiko cha kampuni ya ujenzi ya CRJE, kikiendelea na ujenzi wa barabara ya Tandale kwa Mtogore, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ramaphosa atangaza neema kwa Tanzania

INATOKA UK. 2

kuwa ndiyo mikakati ya ukombozi wa taifa lao ilikuwa ikipangwa.

Alisema kuwa mbali na kusaidia Afrika Kusini, eneo hilo pia limevisaidia vyama vingi vya siasa vya nchi za Afrika kama vile Frelimo, Zanu, Swapo na ANC katika harakati za kudai uhuru.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kufika Morogoro hususan eneo hili la ukombozi, japokuwa kaka yangu alikuwa anaishi hapa, ninajisikia furaha kufika eneo hili, nimekuja kwenye eneo ambalo kwa miaka ya nyuma lilitoa malazi kwa wapigania uhuru wetu, wengine walikuja wakiwa watoto, wengi walizikwa hapa," Rais Ramaphosa alisema.

Aliongeza kuwa ni vema kwa Tanzania na Afrika Kusini kuendelea kushirikiana katika masuala ya kiuchumi, teknolojia na ujuzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema Tanzania iko tayari kufundisha lugha ya Kiswahili Afrika Kusini. Alisema eneo la Solomon Mahlangu limeunganisha undugu wa Tanzania na Afrika Kusini na kwamba Serikali ya Tanzania iliyakarabati majengo yake ili kuimarisha na kuwakumbuka wapigania uhuru.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema: "Kituo cha Solomon Mahlangu ni sehemu ya Afrika Kusini."

# Tanzania, Afrika Kusini kushirikiana maendeleo viwanda

INATOKA UK. 3

kati ya Tanzania na Afrika Kusini pasi na kulitaja eneo hilo.

Waziri Mkuu alisema eneo la Mazimbu limebeba historia muhimu ya kumbukumbu ya vuguvugu la ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini.

"Mheshimiwa Rais, Tanzania ikishirikiana na nchi tano zilizokuwa katika kundi la mstari wa mbele (Angola, Tanzania, Zambia, Botswana na Msumbiji) ilijishughulisha sana katika ukombozi kusini mwa Afrika na katika kukomesha sera za ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini," alisema.

Pia alisema sera za ubaguzi wa rangi zilikoma Februari, 1994 na kufuatiwa na uchaguzi huru na wa haki uliosababisha kupatikana kwa Rais wa kwanza mzalendo wa nchi hiyo, Mzee Nelson Mandela, Mei 1994.

"Tunapozungumzia kukoma kwa sera za ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini, siku zote tutawakumbuka Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Mzee Nelson Mandela kwa utumishi wao uliotukuka kwa kujenga misingi imara ya umoja katika mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini,"alisema.

Alisema misingi imara iliyojengwa na wazee wetu hao, imekuwa chachu ya ushirikiano kwenye majukwaa ya kimataifa hususani katika kupambana na ubaguzi wa kiuchumi na unyanyasaji wa aina mbalimbali.

Waziri Mkuu alisema namna pekee ya kuwaenzi viongozi hao ni kuendelea kujenga umoja na kushirikiana katika kuimarisha Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

# Mabalozi waona fursa uwanja wa ndege Dar

INATOKA UK. 3

Balozi wa Tanzania Sweden, Dk. Willibrod Slaa, alisema kuanza kutumika kwa jengo hilo la tatu la JNIA kutasaidia kuwa na mvuto na kuleta wawekezaji na watalii wengi zaidi na hivyo kukuza uchumi wa taifa.

Alisema ili kufikia malengo tarajiwa, Tanzania inapaswa kujifunza kwa mataifa mengine yaliyofanikiwa kwa sababu haiwezi kufanikisha kila kitu kwa wakati mmoja.

Balozi wa Tanzania Malaysia, Ramadhani Dau, alisema uwanja huo una vigezo vya kimataifa hivyo ni fursa nzuri kwao kuendelea kuitangaza Tanzania duniani kote.

Balozi wa Tanzania India, Baraka Luvanda, alisema fursa nyingi zimeendelea kufungua milango ya uwekezaji nchini hasa kuanza kwa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Mumbai.

"Kuwapo kwa safari hii kumefungua milango ya kukuza uchumi, imerahisisha usafiri kwa raia wa India na Tanzania ambao watazidisha ushirikiano katika sekta mbalimbali," Balozi Luvanda alisema.

Balozi wa Tanzania Cuba, Valentino Mlowola, alisema kuwapo kwa uwanja huo ni hatua kubwa na serikali inahitaji pongezi kwa kufungua milango ya kukuza uchumi.

Alisema Cuba wanatembelewa na watalii milioni tano kwa mwaka, hivyo kuwapo kwa uwanja huo ni kigezo cha kuwashawishi kuja nchini kutembelea vivutio vilivyopo.

Alisema pia watashirikiana na Cuba kujifunza mbinu mbalimbali zitakazowezesha watalii kutembelea vivutio mbalimbali nchini.

Awali, akielezea mradi huo, Mkurugenzi wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Patrick Mfugale, alisema jengo hilo lina uwezo wa kuhudumia watu 2,800 kwa saa moja na watu milioni nane kwa mwaka.

Alisema eneo la maegesho ya ndege linaweza kuegesha ndege 19 za daraja C na 11 daraja E na gharama za mradi huo ni Sh. bilioni 707 na tayari Mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni 680.

# Arusha kinara wa mapato kitaifa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imeibuka kidedea kitaifa baada ya kuvuka lengo la kukusanya mapato ya ndani kwa zaidi ya Sh. bilioni 16 na kuzishinda halmashauri zote.

Aidha, Arusha inamaliza mwaka ikiwa imekusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 105 na kuwa kinara kitaifa, kwa mujibu wa Meya wa Arusha , Kalisti Lazaro.

Meya aliyasema hayo jana alipozungumza na vyombo vya habari na kueleza halmashauri ililenga kukusanya Sh.bilioni

15. 6 lakini imekusanya bilioni 16.4

Alisema Jiji la Arusha limeongoza kwa makusanyo kwa mwaka 2018/19 katika majiji yote nchini.

Awali lengo lilikuwa kukusanya Sh.bilioni 15.6 lakini halmashauri imevuka lengo na kufikia Sh. bilioni 16.4.

Alisema haijawahi kutokea Jiji la Arusha likaongoza kwa mapato ya ndani na hivyo wameweka mkakati ambao utaliwezesha kuendelea kuongoza kutokana na ubunifu wa kuibua vyanzo vingine vya mapato na kuimarisha usimamizi wake.

Alisema katika kuhakikisha wanaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, halmashauri hiyo imekabidhi vyanzo 14 vya mapato kwa Shirika la Suma JKT.

Baadhi ni kusimamia ukusanyaji wa mapato yanayotokana na maliasili na machimbo ya moramu , yote hayo ni kutokana na uadilifu wa chombo hicho cha Jeshi la Kujenga Taifa.

Meya Lazaro, alisema kuwa halmashauri itaendelea kubuni vyanzo vingine vya mapato, ikiwamo ujenzi wa maduka eneo la Ranger Safari, kuboresha machinjio, kumaliza migogoro ya kiuwekezaji.

Alisema kutokana na makusanyo hayo halmashauri imeondoa msongamano wa wanafunzi madarasani na utengenezaji wa madawati kwa kutumia karakana ya halmashauri hiyo na wamekarabati kituo cha afya cha Moshono.

Aidha, alisema mwaka huu halmashauri inajenga shule za ghorofa, kwenye shule za Moivaro, Muriet na Terati kupitia fedha za ndani.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk.Maulid Madeni, alisema kuwa halmashauri imejipanga kukusanya Sh.bilioni 20 kwa mwaka 2019/20.

Alisema ukusanyaji huo utaiwezesha halmashauri hiyo kujitegemea kimapato ikiwemo kulipa mishahara ya watumishi wote na hivyo kuipunguzia serikali mzigo wa kutoa ruzuku kwa halmashauri hiyo.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi huyo amewaonya wafanyabiashara wakubwa wa maduka wanaotumia vitambulisho vya machinga kuendesha biashara zao na atakaowabaini atawachukulia hatua kwa kuwa wanaikosesha halmashauri mapato.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Jackson Sipitieck akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Albert Msole na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Silvanus Tairo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yasifu sekta binafsi kuinua utalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, amesifu ushirikiano baina ya sekta binafsi na Serikali ambao umeinua utalii nchini.

Alitoa pongezi hizo jana kwenye kikao cha wadau wa utalii kilichofanyika jijini Arusha kikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mrisho Gambo.

Alisema katika kuhakikisha sekta hiyo inazidi kuimarika na kuvutia watalii wengi , serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 300 kwa ajili ya kuimarisha miundo mbinu ya ukanda wa kusini.

"Lakini pamoja na haya yote napongeza sekta binafsi sababu ina mchango mkubwa katika kukuza utalii na hivi sasa serikali ina mikakati ya kuimarisha mazingira ya biashara ya utalii naomba tuzidi kushirikiana,"alisema Mkenda.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Arusha , Mrisho Gambo, alisisitiza kwamba ushirikiano baina ya sekta binafsi na serikali katika kuendeleza utalii ni jambo la muhimu na la lazima.

Aidha, Gambo alisema katika kuhakikisha watalii wanaongezeka suala la usalama na ulinzi wa watalii liwe kipaumbele na kutaka Jeshi la Polisi na vyombo vya ulinzi na usalama kudumisha ulinzi ili kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini.

Alitaja changamoto kubwa inayowakera watalii kuwa ni kutumia muda mwingi barabarani kutokana na masuala ya usalama barabarani hali hiyo inachangia watalii kukatishwa tamaa.

Aidha, ulevi wa baadhi ya madereva wanaobeba watalii kuendesha magari yanayobeba wageni hao ni kero nyingine akisema hilo ni tatizo lililokithiri katika mji wa Karatu.

Gambo aliomba kila mdau wa utalii kuhakikisha katika eneo lake wanaweka mazingira rafiki ya kufanya biashara ya utalii kuendelea.

"Sisi serikali tutazidi kujenga mazingira rafiki ya kufanya biashara ya utalii ili uzidi kuimarika,"alisema Gambo.

Mwenyekiti wa chama cha kuhudumia watalii (Tato), Wilbrad Chambulo, alisema changamoto kubwa iliyopo ni watalii kuchelewa kulipia visa katika kiwanja cha kutokana na uchache wa wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji uwanjani hapo.

Alisema wajibu wa Tato ni kubadilisha mawazo ya wadau wa sekta hiyo wanaodhani polisi ni adui wakati sivyo, na kuwaomba kuongeza ushirikiano baina ya polisi na makampuni ya kusafirisha watalii.

"Lakini vituo vilivyojengwa na serikali katika eneo la Kikatiti, Makuyuni, Karatu na njia ya Namanga ni kwa ajili ya usalama wa watalii, hivyo naomba baadhi ya askari wa usalama barabarani msigeuze vituo hivi, kama mtaji wenu na kuwa chanzo cha kuchelewesha watalii inatuharibia soko la utalii nchini,"alionya Chamburo.

# Kijiji chasahau shida ya maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

WAKAZI 650 wa Kijiji cha Sangara wilayani Babati mkoa wa Manyara, wameondokana na changamoto ya muda mrefu wa ukosefu wa maji. wameachana na usumbufu huo , baada ya mradi wa maji uliogharimu Sh.milioni 229 kuzinduliwa jana.

Mradi huo unatoa lita 352,800 kwa siku, sawa na lita 14,700 kwa saa, unahudumia watu kwa utaratibu wa kulipia huduma kabla ya kuipata yanayofanyika kwa njia ya kielektroniki.

Mkurugenzi wa shirika la kimataifa la Water Aid, Abel Dugange, akizungumza kwenye uzinduzi wa mradi huo alisema, waliingia makubaliano ya kutekeleza mradi huo mwaka jana na halmashauri ya Wilaya ya Babati, Shirika la Habitat for Humanity, kampuni ya eWater na taasisi ya fedha ya Unit Trust of Tanzania (UTT-MFI). Dugange alisema kabla ya kutekeleza mradi huo upatikanaji wa maji kwenye kijiji hicho, ulikuwa asilimia 20 tofauti na lengo la taifa la asilimia 85 ya huduma za maji vijijini. "Mradi huu umelenga kuhamasisha ubunifu na kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu na uendeshaji wa miradi ya maji ili kurahisisha upatikanaji wa huduma endelevu na hakika ya maji safi na salama vijijini," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, akizindua mradi huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, aliwataka wakazi wa eneo hilo kuutunza ili uwe endelevu. Kitundu alisema lengo la serikali ifikapo mwaka 2020 ni kuona kuwa asilimia 85 ya watu waliopo vijijini wanapata maji safi na salama na mwaka 2025 iwe asilimia 95 na mwaka 2030 iwe asilimia 100.

Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Vrajilal Jituson, alisema mradi huo ni wa mfano, kwani umeanzia Babati kisha Wilaya za Korogwe mkoani Tanga na Arumeru mkoani Arusha zikafuata.

Jituson alisema mchotaji anaokoa muda kwani anaweza kuteka hata usiku na hauhitaji muuzaji wa maji kuwepo katika kituo kwani huduma imeshalipiwa.

"Inaongeza usalama wa fedha kwani hazitopotea.Utaratibu pia umeongeza nidhamu ya matumizi ya maji kwani hata tone moja linalipiwa," alisema Jituson.

Mkazi wa kijiji hicho Magdalena Bayo alisema awali walikuwa wanachota maji umbali mrefu, kwenye visima na makorongo ila mradi huo umewasaidia kwani upo karibu nao.

"Mradi ni mzuri yaani kama vocha ya simu unaingiza tokeni maji yanatoka kadiri unavyolipia ndivyo unavyopata maji na hatutembei umbali mrefu kama awali unaamka alfajiri unapambana na foleni," alisema.

# Same yalia uhaba watumishi wa afya

**Na Godfrey Mushi,** SAME

IDARA ya Afya ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, inakabiliwa na upungufu wa watumishi 689 wa kada hiyo.

Taarifa ya Halmashauri ya Wilaya hiyo iliyothibitishwa na kuwekwa katika tovuti ya serikali, inaonyesha kuwa idara hiyo inahitaji jumla ya watumishi 1,114.

Sehemu ya taarifa hiyo inaonyesha kuwa Hospitali ya Wilaya inahitaji kuwa na madaktari 23 lakini waliopo ni wanne na upungufu ni madaktari 19, wauguzi wanaohitajika ni 99 na waliopo ni 71, hivyo kuwa na upungufu wa wauguzi 28.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Godfrey Andrew, alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu jana ili kutoa ufafanuzi zaidi kama kuna jitihada zilizofanywa na Serikali kuongeza watumishi hao, hakupatikana kutokana na simu yake kutopatikana hewani.

Aidha katika taarifa hiyo, miongoni mwa changamoto halmashauri inayokutana nayo ni usambazaji wa dawa na vifaa tiba, usioendana na mahitaji na ukosefu wa mara kwa mara wa dawa na vifaa tiba kutoka Bohari Kuu ya Dawa.

Changamoto nyingine ni bajeti ndogo ya fedha za matumizi mengineyo (OC), fedha haziji kwa wakati, jamii kutokuelewa kwamba vituo vya kutolea huduma ni mali yao, kutokuwapo kwa umeme kwa kuaminika, usajili hafifu wa Mfuko wa Afya ya Jamii na upungufu wa wataalam hasa wa maabara katika vituo vya afya na zahanati.

Hadi sasa, wilaya hiyo ina vituo vya kutolea huduma 60, kati ya hivyo 31 ni vya serikali na 29, vinamilikiwa na watu binafsi na mashirika ya dini.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto ya uhaba wa watumshi wa kada hiyo, Wilaya ya Same, ina vyuo viwili vya afya (utabibu na uuguzi) vyenye uwezo wa kudahili wanafunzi 90.



Mtaalam wa masuala ya kijinsia, kijamii na maendeleo kutoka taasisi ya Maendeleo ya Ekama Tanzania, Mary Nsemwa, akizungumza kwenye wasilisho la matokeo ya tathmini na mbinu zinazotumiwa na vikundi vya wanawake katika kuzuia ukatili dhidi ya watoto, lililofanyika katika Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mwenyekiti wa kikundi cha Mshikamano B Vicoba Mbagala, Sophia Chembea na Mwanachama wa kikundi cha vijana cha Karibu Morning Flower Temeke, Salum Tego. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watoto 100 wenye ulemavu waibuliwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAZI ya kuchochea hamasa ya utoaji wa elimu kwa watu wenye ulemavu wenye 'uziwi kutoona' katika Mkoa wa Kilimanjaro, imeanza kuleta matokeo chanya, baada ya Shirika la Sense International Tanzania, kuwaibua watoto 100 waliokuwa wamefichwa kwa kutokubalika katika jamii.

Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, Sura ya 183 na Kanuni zake za Mwaka 2012 zilizotengenezwa chini ya kifungu cha 61 na kuchapishwa Mei 4, 2012 katika Gazeti la Serikali, inaelekeza makundi yote ya watu wenye ulemavu katika jinsia zote na umri wa kwenda shuleni, watakuwa na fursa sawa ya kupokea elimu na mafunzo stadi kupitia mfumo wa elimu jumuishi.

Ofisa Programu wa Shirika la Sense International Tanzania, Benjamin Kihwele, alisema sheria hiyo inaelekeza kwamba ni jukumu la Serikali kuhakikisha watoto wote, vijana na watu wazima wenye ulemavu wanaandikishwa, washiriki kikamilifu na kupata mafunzo stadi na programu zingine za elimu kwenye shule za kawaida, bila kujali namna mbalimbali ya historia ya nyuma na uwezo wao na bila aina yoyote ya ubaguzi.

Kihwele alikuwa akizungumza jana na wataribu wa elimu kata wa Wilaya za Same, Mwanga na Rombo katika kikao kazi kilichofanyika mjini hapa.

"Sheria imeelekeza kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kushirikiana kwa masuala ya elimu ndani ya eneo ambalo shule ipo, kutenga fedha kugharamia gharama za elimu, makazi, chakula, usafiri na gharama nyingine za wanafunzi na wanachuo wenye ulemavu waishio ndani na nje ya eneo hilo.

"Sasa kwetu sisi Sense International, tangu kuanza kwa mradi huu kumekuwa na mabadiliko makubwa yaliyoleta matokeo chanya kwa sababu watoto wengi walikuwa hawawezi kuwasiliana, kutumia mbinu za kuwasiliana na wenzao na jamii kwa ujumla na sasa wanaweza kuwasiliana," alisema.

Mradi huo wa miaka minne, ulioanza kutekelezwa mwaka 2016 utafikia ukomo wake mwaka 2020.

Wakati wa utekelezaji wake, walemavu wenye uziwi kutoona, wengine walikuwa na changamoto za kujimudu kiviungo lakini kupitia watalaam mbalimbali, wanaotoa huduma ikiwa ni pamoja na walimu, wamewasaidia na sasa wanaweza kujimudu kujongea kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na walikuwa pia hawana uelewa au utambuzi wa mazingira wanayoishi na vitu vyote vinavyosaidia katika mfumo wa maisha kuanzia asubuhi mpaka usiku.

Mwezeshaji wa kitaifa wa elimu jumuishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mary Batamula, katika majadiliano na waratibu hao, alisema sera ya elimu jumuishi inatekelezeka, kikubwa ni watu wabadilishe tu mtazamo na fikra zao kuhusu watoto wenye uziwi kutoona.

"Kumefanyika kazi kubwa sana, nyie mnajua kundi la watoto wenye ulemavu wa uziwi kutoona limesahaulika sana katika jamii yetu, ni kundi ambalo halikubaliki, ni kundi ambalo watu wamekuwa na maswali mengi kwamba je, wanaweza kufundishika au wanaweza kufanya nini. Lakini katika kujadili nyie wenyewe bila kuambiwa mmeona kumbe wanafundishika na mmeona kumbe kufundishika au kujifunza kila mtoto anajifunza kutokana na uwezo wake," alisema Batamula

Akieleza mtazamo wake katika kikao hicho, Marietha Shayo ambaye ni Ofisa Elimu, Elimu Maalum wa Wilaya ya Same, alisema baada ya kufanya sensa ya utambuzi na kwa kushirikiana na shirika hilo, wilaya imewatambua watoto 12 katika kata tisa na sasa wanaendelea na masomo na wana msaidizi wa mwalimu.

Alisema yako mabadiliko makubwa kupitia mradi huo kwa sababu mwanzoni watoto hao walikuwa hawapewi nafasi, lakini sasa hivi nafasi yao ni kubwa na wanachangamana na wenzao, wanajifunza na wanaweza kujieleza, jambo ambalo awali lilikuwa gumu, kwa vile walikuwa hawakubaliki katika jamii.

# Madiwani wawakataa watendaji kata

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MPANGO wa kuwang'oa katika nafasi zao watendaji wawili wa kata za Kirua Vunjo Mashariki na Kimochi katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, unasukwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo, baada ya kuwatuhumu kufanya siasa katika ofisi za umma.

Wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika juzi, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Michael Kilawila, alishindwa kuuficha mkakati huo na kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Kastori Msigala, kuwaondoa watendaji hao kutokana na kutokuwa na nidhamu kwa madiwani wanaoongoza kata husika.

"Watendaji hawa wawili wametuhumiwa kwa kujihusisha na siasa katika ofisi za umma, jambo ambalo linasababisha maendeleo ya wananchi kurudi nyuma. Mkurugenzi (Msigala) wakati uchunguzi ukiendelea kufanyika dhidi yao na kwa maslahi mapana ya halmashauri yetu, watendaji hawa waondolewe katika vituo vyao vya kazi na kurejeshwa katika ofisi za halmashauri," aliagiza Kilawila.

Mbali na kuagiza kuondolewa, baraza hilo pia liliwaonya watendaji wengine na watumishi wa halmashauri hiyo ambao wamekuwa wakifanya siasa katika ofisi za serikali, kuacha mara moja.

Kwa mujibu wa Kilawila, watendaji na watumishi wa halmashauri hiyo jukumu lao ni kuwatumikia wananchi kwa muda wote wawapo hapo na si vinginevyo.

Kilawila alisema wako pia baadhi ya watendaji wa kata ambao wamekuwa wakishinda katika ofisi za halmashauri kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na kuhoji ni muda gani wanakaa katika ofisi zao na kusikiliza matatizo ya wananchi.

Akitoa ufafanuzi kuhusu tuhuma hizo, Msigala aliwataka madiwani wanaounda baraza hilo kutambua kwamba kazi ya kuwahamisha watendaji wa Serikali, limekuwa ikiisababishia halmashauri hasara kubwa.

Kutokana na hasara hiyo, Msigala alisema atakutana na watendaji hao wa kata na kuzungumza nao kuhusu tuhuma hizo na kuwasihi kutekeleza jukumu lao la kisheria na si kufanya siasa, lakini pia atafanya uchunguzi wa tuhuma zinazoelekezwa kwao, kabla ya kuchukua hatua ikiwamo kuwahamisha katika maeneo yao ya kazi.






Ofisa Uhusiano Mwandamizi Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Wafanyakazi wa Umma (PSSSF), Rehema Mkamba (kushoto), akiwapa maelezo wananchi walipofika kutembelea banda la mfuko huo, kwenye maonesho ya vijana yaliyofanyika jijini Dodoma jana . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polepole: Acheni mjadala kuongeza muda wa urais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi kimewaonya wanachama wake kuacha mijadala ya kuzungumzia kuongezwa muda wa uongozi wa Rais John Magufuli, kwa kuwa amesema mazungumzo hayo yanamkwaza. Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, ametoa onyo hilo la kuachana na madai ya kumuongezea muda Rais jana.

Aidha, aliwataka viongozi wa chama hicho wasiweke walaghai na wasio na uwezo kuwania nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. Polepole alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Jumuiya ya Wanawake wa Chama hicho (UWT) Taifa , jijini Dodoma. Kwa mujibu wa Polepole, alitwa na Mwenyekiti wa CCM Rais Magufuli na kumtaka awatangazie Watanzania kwamba nchi inaongozwa na katiba na sharia. Alisema Rais alisikia watu wakizungumza kuhusu kuongezewa muda baada ya kumaliza ukomo wa muda wa uongozi wake na kusema ni jambo linalomkwaza.

Alisema muda wake wa kumaliza uongozi ukifika mwisho atang'atuka mara moja na hata ongeza hata dakika tano kwa kuwa uongozi ni mgumu.

"Wale wanachama wenzangu ambao mnaendeleza huu mjadala wa kuongezwa muda wa uongozi naomba muuwache maana Mwenyekiti anasema anakwazwa,"alisema Polepole.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, aliwataka katika kuteua wagombea wajiepushe na walaghai na wasio kubalika na jamii kwa kuwa inawavunja moyo wanawake ambao ni wapiga kura waaminifu.

"Wapiga kura waaminifu ni wanawake lakini tungesema wanaume wakapige kura tungeshaliwa kitambo. Tusiwavunje moyo wanawake kwa kuwateulia wagombea wasio na uwezo,"alisema.

Sambamba na hilo, Katibu alisisitiza kuendelea kuwatumia wanawake kwenye nafasi mbalimbali za uongozi kwa kuwa watalisaidia taifa kupiga hatua zaidi kimaendeleo.

Alisema wanawake hawaibi na wala hawachukui rushwa na pia uwepo wao kwenye maeneo muhimu ni usalama wa taifa kwa kuwa wanajua mengi yanayogusa watu wote. "Wamama hawaibi, hawachukui rushwa ukimuona mama anachukua rushwa jua ana ka boyfriend kanamsukuma. Pia mtoe mawazo yenu kwenye vikao vya maamuzi ili kumsaidia Rais John Magufuli kwenye utendaji kazi yake,"alisema Polepole. Aliagiza UWT kutengeneza kanzi data ambayo itaonyesha wanawake na elimu zao ili waweze kupata nafasi mbalimbali za uteuzi. Awali, Katibu wa UWT Taifa, Queen Mlozi, alisema mabaraza hayo yamekuwa yakilenga kuwainua wanawake kiuchumi na kisiasa huku akisisitiza kuwa wataendelea kumlinda na kumtetea Rais John Magufuli kwa mshikamano wao.

Aidha, alisema katika uchaguzi wa serikali za mitaa watahakikisha wanashinda kwa kishindo kama Tsunami na kuwaomba wanachama wa chama hicho kuendelea kuwa na umoja.

# Tamisema kutokomeza mbu, wadudu dhurifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa kushirikia na Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe imeeleza nia ya kupambana na malaria na dengue.

Hilo litafanywa kwa kutokomeza mazalia ya mbu na wadudu wengine dhurifu wanaoeneza maradhi, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe Dk. Ntuli Kapologwe.

Akizungumza na Nipashe alisema Tamisemi ambayo inasimamia sekretarieti za mikoa 26 na halmashauri 185 itahakikisha wanaweka kwenye bajeti suala hilo.

Alisema katika maandalizi ya mpango wa bajeti unaoanza Oktoba mwaka huu watahakikisha fedha zinakwenda kwenye mapambano dhidi ya mbu na wadudu wengine.

"Dhamira yetu ni kuunga jitihada za Rais John Magufuli za kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya njema na ili dhamira hiyo itimie kila Mganga Mkuu wa Mkoa na Mganga Mkuu wa Halmashauri atakuwa na jukumu la kulifanikisha lengo hilo kwenye eneo lake,"alisema Kapologwe.

Kadhalika, alisema katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Waganga Wakuu unaoanza wiki ijayo Agosti 20-24 mwaka huu wataweka msisitizo mkubwa katika kulinganisha utendaji na uwajibikaji wa waganga wakuu hao katika maeneo mbalimbali.

Alisema ulinganisho huo utafanyika pia katika eneo la kupambana na mbu na wadudu dhurifu.

"Hii idara ina majukumu mbalimbali ikiwamo kuzisimamia sekretarieti na mamlaka za serikali za mitaa ili ziweze kutoa huduma bora za afya, ustawi wa jamii na lishe kwa kufanya uratibu, uandaaji wa mipango na bajeti, usimamizi zaidi na tathimini,"alisema.

# Jafo awaambia vijana wachangamkie mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, ,amewataka vijana kuchangamkia fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri akisema idadi ya vijana wanaojitokeza ni ndogo ikilinganishwa na wanawake.

Alitoa kauli hiyo juzi hapa Dodoma katika maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya Vijana iliyoandaliwa na wadau mbalimbali likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani(UNFPA).

Alisema pamoja na serikali kutunga sheria kwenye utoaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu lakini idadi ya vijana wanaochangamkia fursa hiyo hairidhishi.

"Kuna fursa mbalimbali kwa ajili ya vijana lakini bahati mbaya wachache wanachangamkia mikopo kwenye fedha za halmashauri. Pia hata wanaojitokeza kukopa hawarejeshi tofauti na wanawake ambao wanaongoza kwa kukopa fedha hizo na waaminifu kwenye urejeshaji,"alisema.

Waziri huyo aliwahimiza vijana kulima kilimo cha kisasa kwani kimekuwa na faida kubwa akisema ekari moja ikipandwa vizuri inaweza kutoa mazao mengi.

"Ukifuga kuku wa mayai 10,000 ambao kila siku wanatoa 'trei' 300 inayouzwa Shilingi 7,000 ina maana kila siku wana uwezo wa kupata milioni moja.Vijana naomba niwaambie badilishaneni mawazo,wekezeni katika ujasiriamali badala ya kuwaza kuajiriwa,"alisema.

Aidha, aliwataka vijana kufanya tathmini ya yale watakayokubaliana na kisha wanayapeleka serikalini.

Aliwataka waliopewa nafasi kufanya kazi kwa bidii na kuacha maigizo ili waache historia.

"Hebu igeni mfano wangu mimi simwangushi Rais,bajeti ya nchi zaidi ya asilimia 20 inakuja kwenye Wizara yangu ninasimamia wizara kubwa, vijana mkipewa nafasi fanyeni kazi hakikisha unaacha alama ili wakukumbuke,kijana sio sifa kukaa kiti kirefu halafu unasema kunyweni mpaka mikono idondoke, acha alama wekeni mifano kwa watu wengine,"alisema Jafo.

Waziri Jafo alisema vijana ambao wamepewa fursa wasivunje matumaini ya vijana wenzao.

Pamoja na hayo, Waziri Jafo aliwataka vijana kujitambua kwa kuhakikisha wananunua bidhaa zinazozalishwa na vijana wenzao.

"Tuna agenda kubwa tupambane na adui wa roho mbaya kuna vijana wengine wana roho mbaya wapo kuwakwamisha wenzao kwanza tupendane,bidhaa hizo zote kama tutanunua tutaenda mbali kwani vijana ni timu kubwa,"alisema.

Naibu Katibu Mkuu,Wizara ya Vijana,Sanaa,Utamaduni na Michezo,Zanzibar,Amour Hamil Bakari,alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kufanya juhudi ili vijana wapate pamoja na kufanya kazi zenye staha.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA hapa nchini, Jacqueline Mahon, alisema siku hiyo inaadhimishwa ili kutambua mchango muhimu wa vijana katika kuleta maendeleo na kujadili changamoto zinazowakabili ili zipatiwe ufumbuzi.



# Mwitikio uzazi wa mpango changamoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIWANGO cha matumizi ya uzazi wa mpango Zanzibar kimeelezwa kuwa ni kidogo kutokana na mitazamo hasi kwa jamii kuhusiana na huduma hizo.

Imeelezwa kuwa hali hiyo imesababisha kiwango hicho kuwa asilimia 14, hali ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kudumaza maendeleo ya wanawake na watoto. Ofisa wa Elimu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Batula Abdi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzazi wa mpango na kulinda afya ya mama na mtoto.

Abdi alisema kutokana na kuwapo changamoto hiyo, juhudi zinahitajika katika kutoa elimu na kuachana na dhana potofu katika msimamo wa uzazi wa mpango.

Alivitaja baadhi ya vikwazo vikubwa vinavyochangia hali hiyo kuwa ni uelewa mdogo kuhusu imani ya dini na maamrisho yake katika vitabu vitakatifu vya dini.

Ofisa huyo alisema pamoja na dhana hiyo, dini ya Kiislamu haijakataza familia kujipangia na kufuata uzazi wa mpango ambao lengo lake ni kukuza familia.

"Wakazi wa Zanzibar asilimia 90 ni Waislamu hivyo dini ya Kiislamu haijakataza uzazi wa mpango. Uzazi wa mpango lengo lake kulinda familia na ukuaji bora na siha njema," alisema.

Pia alisema kazi kubwa inayofanywa na UNFPA ni kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha jamii hasa wanawake na watoto, inakuwa na afya njema.

Naye Ofisa Kitengo cha Afya kutoka UNFPA, Dk. Azzah Nofly, alisema uzazi wa mpango ni mzuri na unawaweka wanawake katika hali nzuri ya afya kwa asilimia 45 na kushiriki kikamilifu shughuli za maendeleo.

Alisema kisiwa cha Pemba kipo chini zaidi katika elimu ya uzazi wa mpango kwa asilimia saba zaidi katika Wilaya ya Mkoani.

"Utafiti wetu umeonyesha kwamba kisiwa cha Pemba wananchi wake hawana elimu ya uzazi wa mpango, hivyo ziko familia zinakabiliwa na hali ngumu ya maisha," alisema.

UNFPA inashirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar kuhamasisha jamii kuwa na mwamko ya kuimarisha uzazi wa mpango kwa ajili ya kulinda afya za watoto na wanawake.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Martha Luleka (wa kwanza kushoto). Wengine pichani ni Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri (wa pili kusho) na kulia ni Mbunge wa Jimbo la Sikonge, Joseph Kakunda. **PICHA: WIZARA YA ARDHI**

# SADC yasifu maendeleo utalii Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UJUMBE wa wananchama wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umetembea Zanzibar na kuridhishwa na maendeleo ya sekta ya utalii pamoja na juhudi za kulinda historia ya nchi.

Dhlamina Nkoso kutoka Swaziland, mmoja wa wajumbe hao, alisifu juhudi za kuitangaza Zanzibar katika sekta ya utalii duniani na kusema Zanzibar inauzika katika soko ya utalii kutokana na historia na majengo ya kale.

Alisema amepata nafasi ya kutembelea visiwani vingi duniani na kuijumuisha Zanzibar miongoni mwa visiwa vyenye historia na maeneo ya kuvutia katika utalii.

Baadhi ya maeneo waliyotembelea wageni hao ni kanisa la Mkunazini ambalo lilikuwa soko la watumwa pamoja na mahandaki ya chini kwa chini yaliyoko Hurumzi eneo la Mji Mkongwe.

Akizungumza na ujumbe huo, Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, alisema Serikali ya Zanzibar imejipanga katika kulitumia soko la nchi za (SADC) katika biashara za aina mbalimbali kwa wananchi wake wakiwamo wajasiriamali.

Alisema hivi sasa tayari wafanyabiashara kutoka Zanzibar wanalitumia vizuri soko la dagaa lililoko Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Hafidh alisema mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sasa ni kuimarisha soko la bidhaa za viungo kama vile pilipili manga, pipilipi hoho na uzile.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunalitumia soko la SADC kwa ajili ya kuuza bidhaa za viungo ambazo zinapatikana kwa wingi nchini," alisema.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Dk. Abdalla Juma, alisema miongoni mwa mikakati inayochukuliwa kwa sasa ni kuitangaza Zanzibar katika ramani ya dunia ya utalii.

"Tunataka kujitangaza zaidi katika soko la SADC kwa wananchi wetu ili kufaidika na fursa ziliopo za vivutio vya utalii," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohamed, alisema amefurahishwa na ujio wa wajumbe kutoka SADC ambao wameziona fursa mbalimbali zilizoko Zanzibar.

# Bima kwa wakulima, wavuvi zaanzishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango Zanzibar imesema serikali za Zanzibar na Muungano zimefungua fursa za uanzishwaji wa bima ndogo kwa wananchi wa kipato cha chini wakiwamo wakulima, wavuvi na wafugaji ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

Waziri wa Wizara hiyo, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, alisema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa tano wa kujadili huduma ndogo za bima unaofanyika mjini Zanzibar.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuhamasisha wananchi wa kipato cha chini kulipa umuhimu suala hilo ambalo limeonekana kwa Tanzania kuwa makundi hayo mengi hayajazifikia huduma hizo.

Balozi Ramia alisema sekta ya bima ina mchango mkubwa wa kusaidia kukabiliana na matatizo mbalimbali yakiwamo majanga na kuongeza pato la taifa, hivyo ni vyema Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) na taasisi zake kuhakikisha inawaelimisha wananchi ili kutumia huduma hizo ipasavyo.

Sambamba na hayo, Ramia alitumia fursa hiyo kuitaka TIRA kuhakikisha inaweka sera nzuri za kuongoza taasisi hizo ili kuleta tija kwa jamii.

Kwa upande wake Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Mussa Juma, alisema mamlaka hiyo na kampuni zake zimeweka msisitizo mkubwa ili kuona wananchi wa chini wanatumia huduma hiyo ipasavyo kwa ajili ya kuwasaidia wao na taifa kwa ujumla.

Alisema wananchi wa Tanzania bado wana uelewa mdogo wa kuzitumia bima hizo, hivyo malengo yao ni kuwajengea uwezo ili kuongeza uzoefu wa kujiunga na huduma hizo.

Dk. Juma alisema idadi kubwa ya wanajamii hukutwa na matatizo au majanga mbalimbali katika shughuli zao za kila siku, hivyo huduma bima itakuwa chachu ya kuwasaidia kujikwamua na matatizo hayo pale yanapotokeza.

Mwakilishi wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC), Aberhard Mbepera, alisema mara nyingi bima huchukuliwa kwa makundi mengine ikiwemo wafanyakazi na wafanyabiashara lakini kundi la kilimo bado lipo nyuma katika kutumia huduma hizo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Kampuni za Bima, Khamis Suleiman, alisema lengo la mkutano huo ni kuangalia uzoefu kwa nchi zingine ambazo zimefanikiwa katika utumiaji wa bima ndogo.

Alisema bima ndogo zina mchango mkubwa wa kumsaidia mwananchi wa chini kujitegemea pamoja na kuinua pale anapopata maafa.

Mkutano huo wa siku tatu wa kwanza kufanyika Zanzibar, unahudhuriwa na zaidi ya washiriki 300 kutoka zaidi ya nchi 50 za barani Afrika, ukiwa na kaulimbiu "Muundo wa Biashara ya Bima Shirikishi kwa Afrika".



Soma UK. 15

KIBA

JUMAMOSI AGOSTI 17, 2019

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI

# RIP MBALAMWEZI



UK.14

## BASI SAWA



# Aslay, Sunny wajiachia watu 'Waone'

WAKATI mkali wa Bongofleva, Aslay anatamba na kibao chake 'Chuki', sasa amekuja kivingine akiwa na mrembo Sunny.

Wasanii hao wametambulisha kazi yao mpya inayoitwa 'Waone' ambayo imeanza kuwapagiwisha mashabiki wa muziki nchini.

Ujio wa video hiyo ya wimbo mpya imesababisha kuwapo na maoni tofauti kutoka kwa wafuasi wake, baadhi wakimpongeza kutokana na kazi hiyo nzuri.



# AT kastaafu muziki?

HOFU imetanda kwa mashabiki wa msanii wa muziki wa mduara, AT, ambaye inadaiwa ameachana na kazi ya muziki huo na badala yake kumrudia Mungu.

Mwanamuziki huyo ambaye alitamba na vibao mbalimbali ikiwamo 'Nipigie' amekuwa kimya kwa muda mrefu jambo ambalo limeibua mjadala mkali mitandaoni.

Kuna baadhi ya watu wa karibu na msanii huyo wamedai AT ameachana na habari ya muziki na badala yake amemrudia Mungu kwa kufanya ibada.



# KIFO CHA UTATA
# Nani kamuua Mbalamwezi?

UTATA umeibuka baada ya kifo cha msanii wa kundi la The MAFIK aitwae Mbalamwezi ambapo baadhi ya ndugu wamesema kwamba mwili wake ulikutwa maeneo ya Africana Dar es salaam ukiwa hauna nguo.

Mwili wake uliokotwa baada ya siku kadhaa ya kutoweka na hakuna taarifa ya watu kuhusika na kifo hicho.

Akizungumza na Ayo Tv, kiongozi wa kampuni ya utayarishaji muziki ya Kwetu Studio, Fredy Feruzi amesema kabla ya kuokotwa mwili wake vitu vyake ikiwamo gita lake viliokotwa maeneo ya Mbezi Jogoo.

"Vitu vya awali kuokotwa ni gita na vitambulisho vyake, baada ya siku tatu tuliambiwa kwamba kuna mwili wa Mbalamwezi umetupwa eneo Africana ukiwa hauna nguo," amesema Feruz.

Hata hivyo, amesema mwili wake ulikuwa umeharibika sana na kwamba hawajui nani anahusika na kifo hicho au mazingira yake.

## INSTA-TWITTER





**Kila** aliyeko duniani kipo kitu cha thamani ndani yako Mungu amekuwekea ,hata kama watakuona mtu wa ovyo namna gani, amini nakuambia wewe una kitu cha thamani sana. -**Muna Love**.



**Ukialikwa** kwa watu, basi jishughulishe. Hata ukiondoka wanakukumbuka-**Monalisa**.



## Kolabo ya Kiba, Aslay pasua kichwa

NGOMA itakuwaje? Ndivyo swali gumu ambalo mashabiki wa muziki wanajiuliza kuhusu kile kinachodaiwa kolabo ya mastaa Ali Kiba na Aslay.

Wiki hii katika ukurasa wa Instagram ya Kiba aliposto video fupi ikiwaonyesha wawili hao wakiwa pamoja jambo linaloashiria kuna kitu kinakuja punde.

Baada ya kusambaa kwa video hiyo baadhi ya wafuasi wao wamekuwa wakijiuliza namna ngoma hiyo mpya kama itaweza kuwaunganisha na kuwashika mashabiki wao.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...



# LULU JAMES

## Anayetamani Bongofleva kupaa Uingereza

**Na Faustine Feliciane**

LULU James 'Lulu' aliondoka nchini Tanzania miaka 22 iliyopita na kwenda kuungana na mama yake mzazi Uingereza akiwa na miaka sita tu.

Kuishi nchini humo kwa sehemu kubwa ya umri wake kulimpa nafasi ya kujifunza mambo mengi na kuzoea tamaduni na maisha ya Ulaya.

Hata hivyo, kipaji chake cha muziki kimemfanya kuikumbuka nchi yake ya asili (Tanzania) na kuamua kuja kuunganisha nguvu kuhakikisha Tanzania inazidi kufahamika kupitia sanaa ya muziki.

Mzaliwa huyo wa mkoani Arusha kabila la Kimasai tayari ameshaandaa wimbo akiwa hapa nchini ambao amerekodi maeneo ya Mto wa Mbu kwenye studio za Mosquito Records chini ya projuza Fadhir Said 'Faza'.

Nyimbo hiyo inayoitwa Zenzima ambayo vionjo vyake vimewekwa nchini Uingereza, ameiboresha zaidi kwa kuamua kuweka katika maadhi ya Afrika.

"Mimi ni Mmasai, ingawa niliondoka nikiwa mdogo sana hapa Tanzania, bado nafahamu huku ndipo chimbuko langu, wimbo wa Zenzima nimeweka vionjo vya nyumbani Afrika ili kuweka kitu tofauti," anasema Lulu.

Anasema bado Tanzania haijapiga hatua kubwa sana kwenye muziki ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika kama Nigeria na Afrika Kusini.

"Utofauti nilioouona, Serikali za wenzetu kama Nigeria wanawasapoti wanamuziki wao kwa kuweka mifumo mizuri ambapo wasanii wanaona matunda yao na nchi pia inapata mapato kupitia muziki, Tanzania pia inapaswa kuiga mfano huo,' anasema Lulu.

Msanii huyo anasema kabla ya kuamua kurudi nchini, tayari ameshaachia nyimbo tofauti ambazo zinafanya vizuri.

Baadhi ya nyimbo za Lulu ambazo zipo kwenye mtandao wa Yotube ni pamoja na 'It's the time', Be Safe pamoja na ule alioshirikishwa na Jon Hopkins wa 'We Disappear'.

Lulu anaamini Tanzania kuna vipaji na uwezo mkubwa lakini mfumo uliopo sio rafiki kuweza kufahamika haraka.

"Wapo wasanii wa hapa wanafanya vizuri, msanii kama diamond na wengine angalau wameweza kuvuka mipaka ya Tanzania, lakini bado wanahitaji kupata sapoti ya serikali kuweza kufika mbali zaidi," anasema.

Anasema kutokana na ujio wake hapa nchini anaamini kufanya nyimbo kwa kushirikiana na wasanii wa hapa nchini kutasaidia kuivusha Bongo fleva nje ya Afrika.

"Kabla sijaja hapa mwaka 2017 nilikuwa sijui kama kuna Bongofleva, hii inatokana kutokuwa na daraja la kuwapo wasanii hapa na kuwafikisha nje ya Afrika japowapo wanaojitahidi kufanya hivyo.., naamini kwa kushirikiana na wasanii wa hapa tukatengeneza nyimbo nzuri tunaweza kuitangaza zaidi bongo fleva," amesema Lulu.

"Wapo wasanii ambao tayari tumefanya mazungumzo ya kutoa nyimbo za pamoja, yupo Frida, Dama Soul na pia natamani na nina mpango wa kufanya kazi na G-Nako," ameongeza.

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Sio** kila mtu ana uwezo wa kuona uwezo mkubwa ulionao kama unavyotaka. Sio kila mtu anaweza kuona ukubwa wa kipaji ulichokibeba ndani yako. Sio kila mtu anaweza kuona maono uliyobeba ndani-**Johari**.



**Waliotangulia** sasa hawapo lakini hadithi zao tunazo. Waliokuwa na subira za maisha waliishi kwa muda mrefu. Waliokuwa na papara za maisha waliishi kipindi kifupi sana-**Ali Choki**.



**Kila** mtu ana kitu cha kipekee ndani yake kilichotofauti na mwenzake, upekèe huo ndio nguvu yako ilipolalia maana uko peke yako-**Irene Paul**.

# Kuumba!



# BONGOFLEVA KULIKONI?

## WENZENU WANAZOA MAMILIONI, NYIE KILIO

MUZIKI wa Bongo bwana! Tumezoea kuona kila kona ni vilio tu, kuanzia wasanii hadi watengeneza muziki maarufu kama maprodyuza wakilalamika kuibiwa kazi zao.

Sio jambo la kushangaza kusikia mwanamuziki fulani akilia kuibiwa wimbo, lakini ukimuuliza atachukua hatua gani? Hana jibu badala yake atakuambia anamuachia Mungu tu.

Kibaya zaidi wizi huo umewakumba pia watengeneza muziki maarufu kama maprodyuza, nao wanalia kuibiwa kazi zao na wanamuziki ambao wanatumia bila ruhusa yao.

Vilio vya aina hiyo vimezidi kuutesa muziki wa Bongo Fleva kiasi ambacho sasa imefikia mwenye nguvu ndiye anayechukua kila kitu, hakuna atakayethubutu kumnyooshea kidole.

Lakini nchini Marekani, mambo hayo hayapo kwani ikithibitika umeiba wimbo au ala za muziki basi utakachokipata lazima utasimulia hadharani.

Wiki hii wanamuziki maarufu Cardi B, French Montana na Yo Gotti wameshtakiwa na DJ mkongwe nchini Marekani aitwaye, DJ JMK kwa tuhuma za kutumia mapigo ya muziki bila ruhusa yake.

DJ JMK amefungua kesi dhidi ya mastaa hao, akidai kuwa French Montana na Yo Got, Cardi B na City Girls walitumia mapigo yake yaliyotumika kwenye wimbo “Choppa Style” ulioimbwa na Choppa kwenye nyimbo zao za “Oh Yeah” na “Twerk”.

DJ huyo amesema kuwa awali alishafanya mawasiliano na mastaa hao, Na waliahidi kuwa watamlipa lakini mpaka sasa hawajamlipa.

DJ huyo amesema kuwa yeye ndiye aliyetengeneza muziki huo mwaka 2000 na alikuwa anatumia kwenye klabu, Kabla ya kumruhusu Choppa kutumia kwenye wimbo wake wa “Choppa Style”.

Wimbo wa Choppa Style ulitoka mwaka 2002 na upo kwenye album ya ‘Straight From The N.O” ya rapa Choppa. Kwasasa wimbo huo umetazamwa mara milioni 9 kwenye mtandao wa YouTube.

# WANAMUZIKI WAGUMU KUHAMA BENDI

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliwaangalia wanamuziki ambao kwao kuhama bendi moja na kwenda nyingine ilikuwa ni kazi rahisi sana kama vile kumsukuma mlevi.

Wao hawakuangalia athari ambazo bendi inaweza kuzipata wanapohama, au kuwasononesha mashabiki, badala yao waliangalia zaidi maslahi.

Wanamuziki hao ambao waliiongoza kwa kuhama mara nyingi zaidi Bongo ni Adam Bakari ‘Sauti ya Zege’, Shaaban Dede, Athumani Momba na Kassim Mponda ambao wote ni marehemu.

Mwanamuziki ambaye pekee yuko hai kwenye orodha hiyo ni Mhina Panduka ‘Toto Tundu’

Leo tuna wanamuziki ambao walikuwa na roho ngumu. Walikuwa wagumu kuhama kwenye bendi zao licha ya kwamba kulikuwa na majaribio kadhaa ya kutaka kuwachukua, lakini wakang’ang’ana hapo hapo na sababu kubwa ilikuwa ni kutotaka kuwakera na kuwaudhi mashabiki wao, lakini pia wengine walizuia.

**Tx Moshi William-Msondo Ngoma Music Band**

Mwanamuziki kipenzi kabisa cha Wana Msondo Ngoma ambaye hawakukubali hata chembe ahame.

Mashabiki wa Msondo walitumia mbinu mbalimbali kuhakikisha haondoki na walifanikiwa hadi waliposhindwa kufanya chochote, Mwenyezi Mungu alipomchukua mwaka 2006.

Alikaa kwenye bendi ya Msondo kwa miaka 24 bila kuhama, ingawa kulikuwa na majaribio ya hapa na pale yaliyoshindwa.

Katikati ya miaka ya ‘80 akiwa anakaribia kutambulishwa kwenye onyesho la DDC Mlimani Park ukumbi wa DDC Kariakoo, alinyakuliwa kama kifaranga na mashabiki wake waliovamia hapo na kukodi Taxi, kumpeleka kwenye ukumbi wa DDC Keko ambako Msondo walikuwa wakifanya onyesho.

Mashabiki pia walizima jaribio la TX Moshi William kwenda nchini Kenya kuziba pengo la George Peter wa Simba Wanyika baada ya kufariki mwanzoni mwa miaka ya ‘90. Kumbuka Moshi aliathiriwa na sauti ya George kiasi cha kuiiga vizuri sana na hata ukizisikiliza huwa hazina tofauti sana.

Wilson Peter, kaka wa George, alishindwa jaribio la kumvuta Moshi na kutafuta mtu mwingine.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, TOT Plus ilikaribia kumnyakua baada ya kumpa gari na kumvutia maji nyumbani kwake, lakini wadau wa Msondo walizima jaribio kwa kurudisha gharama zote na pia kumnunulia gari lingine.

**Nasri Lubua-DDC Mlimani Park Orchestra**

Ni mwimbaji wa sauti ya kwanza aliyejiunga na Sikinde kutoka Lola Africa mwaka 1985 kuziba nafasi ya Hassan Rehani Bitchuka aliyekuwa ametimkia Orchestra Safari Sound (OSS) ya mtindo wa Ndekule.

Aliiziba vizuri nafasi hiyo na hata Bitchuka aliporejea tena Sikinde aliendelea kuwapo hadi alipohama kurejea Msondo Ngoma mwaka 1990. Nasri ambaye awali alijulikana kwa jina la Francis Lubua aliendelea kukaa kwenye bendi hiyo licha ya kwamba waimbaji wengine walikuwa wakiingia na kuhama hadi alipofariki dunia mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**Abdul Ridhwani ‘Pangamawe’-Msondo Ngoma Music Band**

Huyu ni mpiga gitaa la solo kwenye bendi ya Msondo Ngoma. Alijiunga na bendi hiyo akiwa na umri wa chini ya miaka 18 mwaka 1980 akiwa kama mpiga kinanda baada ya kuondoka kwa Waziri Ally kwenda kuanzisha bendi iliyokuja kujulikana zaidi kwa jina la Njenje.

Baadaye akahamia kwenye gitaa la bass kwa muda mfupi, lakini akageuka kuwa mpiga gitaa la solo wa kutegemewa, akirithi mikoba ya Kassim Mponda baada ya kuihama bendi hiyo na kwenda Sikinde. Hadi leo ni miaka 39, bado yuko na bendi hiyo akiendelea na kazi ya muziki.

**Habib Abbas-DDC Mlimani Park Orchestra**

Ni mmoja wa waanzilishi wa bendi ya Mlimani Park Orchestra mwaka 1978. Wanamuziki wote waanzilishi waolitoka kwenye bendi hiyo wengine wakarejea na wengine wamefariki dunia, lakini Habib Abbas Jeff Mgalusi yeye bado yupo na bendi hiyo hadi leo. Ni mpiga drums tegemeo wa bendi hiyo aliyejiunga akitokea bendi ya Afro 70 ya Patrick Balisidya. Ameitumikia bendi hiyo kwa miaka 41 sasa.

**Said Mabera-Msondo Ngoma Music Band**

Mkurugenzi na kiongozi wa bendi ya Msondo Ngoma. Ndiye mwanamuziki aliyeweka rekodi ya kukaa kwa muda mrefu kwenye bendi moja nchini mpaka sasa. Amekaa Msondo kwa miaka 45 sasa.

Alijiunga na bendi hiyo mwaka 1974 akitokea National ya Arusha akiwa na Bitchuka. Awali Mabera alikuwa akipiga trumpet, lakini aligeuka kuwa mpiga solo namba moja wa bendi hiyo, na hiyo ni baada ya kuchukua mikoba ya Abel Bathazal aliyeiacha bendi na kwenda kuunda Dar Intenational mwaka 1977. Pamoja kurithi gitaa, lakini pia alirithi na uongozi wa bendi hadi leo hii.



Tx Moshi William

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA




**TUMA MESEJI - 0773 477311**




# Dada aliyegeuka mke na hawara kuwa dada

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA anayejua kesho itakuwaje. Ndiyo maana waswahili wakaja na msemo unaosema, binadamu hupanga, lakini Mwenyezi Mungu hupangua.

Kuna wengine wanasema mipango si matumizi. Hiki ndicho kinachoonekana kwenye filamu ya 'Kesho Yangu'.

Imechezwa na wasanii Zuberi Mohamed 'Niva', Richard Mshanga, Sonattah Abdallah Nduka, Jasmin Makema, Gosbeth Mvungi na wengineo. Sonattah aliyecheza kama Lola ni msichana mwanafunzi wa sekondari, anayelelewa na mama wa kambo.

Mama huyo ni kati ya wale mama wa kambo wasiokuwa na huruma na watoto wa wenzao. Anamtesa kupindukia. Pamoja na mzee Mshanga aliyecheza kama Kasongo Matata kumuonya mkewe mara ya kwa mara, lakini ikawa kazi bure.

Anaamua kupanga mpango na mmoja wa daktari asiye na maadili, kumpa mchanganyiko wa madawa uliogeuka kuwa sumu ili kwenda kumuwekea mumewe afe. Lengo ni kudhulumu na kuhodhi mali yote, akihofia kupoteza haki, kutokana na mzee Kasongo kupenda mno binti yake.

Sumu aliyowekewa mzee huyo kwenye juisi inafanya kazi iliyokusudiwa.

Shani, mke wa mzee Kasongo anamkimbizia mgonjwa wake kwa daktari yule yule ili asipate matibabu na hatimaye anafariki dunia. Kinachoendelea kilitarajiwa. Shani anamtimua Lola ili auze nyumba na mali zote za mumewe.

Wanapelekana mahakamani kila mmoja akiwa na wakili wake.

Usia ulioandikwa na mzee Kasongo wakati yuko hai kuwa mkewe huyo Shani ndiye mrithi wa mali zake, unahitimishwa kesi hiyo. Lola anaondoka kwao na mama yake wa kambo anauza nyumba. Aliyeuziwa nyumba ni kijana mmoja Niva aliyetumia jina la Apha.

Wakili Mvungi aliyesimamia kesi ya Lola anaamua kumchukua binti huyo na kuchukua jukumu la kumsomesha. Lola anasoma na hatimaye naye anakuwa mwanasheria. Hata hivyo, lengo la wakili huyo ni kumsomesha binti huyo, amalize masomo yake, hatimaye aweze kumuoa. Lakini alisubiri kwanza.

Kuitana kaka na dada kumlimfanya achelewe kumwambia.

Lola anakutana na kijana Alpha. Kijana huyo pia ni mwanasheria.

Siku moja akaamua kumpeleka nyumbani kwake. Binti anashangaa kufikishwa sehemu ambayo zamani kulikuwa nyumbani kwao.

Anamsimulia Alpha kisa chote cha nyumba hiyo. Kwa sababu wote wa wanasheria wanaamua kuifufua upya kesi ya miaka sita iliyopita. Inabainika kuwa mzee Kasongo hakufa kwa presha, bali ni sumu. Ni mchezo mchafu uliochezwa na daktari na mke wa marehemu. Pia kesi haikuendeshwa kwa haki. Kumbe hakimu wa kesi hiyo ni baba mzazi wa Alpha. Baada ya Alpha na Lola kuwakusanya wahusika wote ambao walikiri kufanya udanganyifu, hatimaye mali zote zinarudi kwa binti huyo.

Alpha anakubali kumuachia Lola nyumba aliyenunua kutoka kwa Shani, bila kudai kurudishiwa pesa alizonunulia.


Kilichofuata hapo ni kwamba Alpha alimwambia Lola kuwa anampenda na anataka kumuoa. Binti anampeleka kwa kaka yake aliyemlea wakili Mvungi. Jasho lilimtoka. Alitegemea kuwa yeye ndiye atamuoa. Alikuwa akisubiri siku muafaka ifike amwambie. Lakini akatoa idhini binti aolewe. Pamoja na hayo alimweleza Lola mpango wake huo alioupanga kwa muda mrefu, lakini kosa lake hakumwambia mapema.

Lola anapelekwa kutambulishwa kwa kina Alpha. Kinachotokea huko ni kwamba baada ya mama mkwe kubaki na binti na kumuuliza maswali kadhaa, inagundulika kuwa yule alikuwa ni binti yake. Picha za marehemu Kasongo alizokuwa nazo mama huyo zilidhihirisha hilo.

Mama alimweleza binti kuwa alizaa mtoto wa kike na mze Kasongo, lakini hawakuweza kuoana kutokana na itikadi za imani.

Baadaye mzee Kasongo alioa mke mwingine na kupata uhamisho na kumchukua mtoto akiwa mdogo, huku yeye naye akiolewa na mwanaume mwingine.

Kwa hadithi hiyo tu jinsi ilivyo ni kwamba Alpha na Lola ni mtu na dada yake. Ndoa hapo hakuna tena. Lola anarejea kwa 'kaka' yake wakili Mvungi. Kutoka kuitana kaka na dada sasa wanageuka kuwa mume na mke. Alpha aliyekuwa mpenzi wake, yeye ni kaka yake wa damu.



# BAHATI YAKE

## ASAP ALIPA FIDIA KUWA HURU

HATIMAYE rapa wa Marekani, Asap Rocky, amekutwa na hatia ya kujeruhi na kisha kuhukumiwa kulipa fidia ya Sh.milioni tatu.

Hukumu hiyo iliyotolewa na mahakama moja nchini Sweden imekuja wiki kadhaa ya vuguvugu lililoanzishwa na wasanii wa

nchi hiyo pamoja na Rais wao Ronald Trump wakitaka msanii huyo kuachiwa huru.

Inaripotiwa kuwa Mahakama hiyo imemkuta na hatia Asap na wenzake wawili kwenye kesi iliyokua ikimuandama ya kumpiga na kumjeruhi shabiki mmoja nchini humo mnamo Juni 30 mwaka huu.

Inaelezwa kuwa Mahakama imeamua kutompa kifungo cha jela na badala yake iliamuru amlipe fidia ya kiasi hicho cha fedha kijana huyo kutokana na kumjeruhi.

Hata hivyo imeripotiwa kuwa Mahakama imeamua kufanya hivyo kutokana na kudai kuwa Asap alisota rumande kwa muda mrefu na ugomvi huo haukusababisha maafa makubwa ya kufikia hatua ya kumpa kifungo.

Rais Donald Trump aliwahi kuingilia kati kuhusu kesi hiyo huku akiitaka serikali ya nchi hiyo kuingilia kati ili aachiwe huru, lakini uongozi wa Sweden ilikataa kuingilia uhuru wa Mahakama.

Wasanii kadhaa walijitokeza kuomba mwenzao kuachiwa aikiwamno Snoop Doggy, Kanye West na mkewe Kim Kardashian.


# Davido waletee watakuelewa tu




MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Davido, ameonekana hana utani na kazi yake kwani baada ya kuidondosha kolabo ya 'Blow My Mind' na mkali wa miondoko ya RnB Chris Brown, sasa anakuja na nyingine kali inayowaunganisha wasanii hao.

Davido amepost kupitia Instagram akiwa kwenye video call na Chris Brownna kuandika 'Another One' akimaanisha nyingine.

Inaripotiwa kuwa Davido ameshaingia studio na kufanya ngoma mpya na wakali kutokea Marekani akiwemo mwimbaji na mwigizaji Ludacris, mtoto wa Diddy (King Combs) na mtayarishaji wa muziki Timberland.



## Burna Boy si kwa Tattoo hizo

STAA wa muziki wa Nigeria, Burna Boy, hatimaye ameamua kuielezea michoro ya tattoo katika mafanikio yake ya muziki.

Akizungumza katika mahojiano hayo yaliyowavutia watazamaji wengi, mwanamuziki huyo amesema kila mchoro una maana kwake na kumfanya kuwa na furaha pale anapotazama.

Katika kile kilichowashtua wengi ni baada ya kuonyesha mchoro wenye jina la mwanamuziki wa zamani wa nchi hiyo, Fela Anakulapo Kuti na kueleza ndiye msanii anayemheshimu kwa sasa.

## Toyin yamekukuta yapi tena?

MASHABIKI wa mwigizaji Toyin Aimakhu, wamekumbwa na hofu baada ya akaunti ya Instagram ya msanii huyo kufutwa picha zote.

Hakuwekwa wazi kwa nini staa huyo wa filamu ameamua kufuta picha hizo katika tukio hilo lililotokea hivi karibuni.

Kabla ya kuamua kuzifuta picha hizo, ukurasa wa msanii huyo ulikuwa na jumla ya wafuasi milioni 3.3 na ulikuwa hai kila siku jambo ambalo limezidisha wasiwasi kwa mashabiki wake.





## Upendeleo wanukia BBNaija

SHINDANO la Big Brother Nigeria, linazidi kuchanja mbuga, lakini mambo yanaonekana kuwa moto baada ya aliyekuwa mshiriki mwaka uliopita Gifty Power, kulalamika kuwa Sayi anapendelewa ndani ya jumba hilo.

Kulingana na madai yake, Gifty amepoteza sifa ya kuishi katika nyumba hiyo baada ya kuwakosea heshima washiriki wenzake Thelma na Ike.

Gifty amesema kutokana na mwendeshaji wa shindano hilo 'Biggie' kufumbia macho suala hilo ladha yake inazidi kupungua kutokana na watazamaji kuona kuna mtu anapendelewa.

## Nick umelianzisha tena kwa Rick Ross

RAPA mwenye vituko vingi, Nicki Minaj ameibua utata mwingine baaada ya kuita mkongwe wa muziki huo Rick Ross kuwa ni takataka.

Swali lililoulizwa na Joe wakati akihojiwa lilionekana kumkwanza mwanadada Nicki Minaj baada ya kumuuliza kwamba ni nani mkali kati ya The Game na Rick Ross? "Hebu usiniletee hapa hiyo takataka, usinifanye nianze kumuongelea. mtu yeyote anayemtukana mtoto wa kike ili kuuza vinakala 250 vya albu, usimlete kabisa mbele yangu," amesema Nicki Minaj



SAFU



## MIONZI YA SHERIA

# Yakuzingatia kwenye biashara ya mizigo

Na John Juma
0716217615

HIVI ni ruhusa au pengine ni haki, kukataa kupokea mzigo ikiwa haufanani na ulioagizwa?

Inawezekana kabisa kwa mujibu wa Sheria ya Uuzaji wa Bidhaa Tanzania Sura ya 214 ndiyo inaelekeza na kuchanganua miamala ya biashara kwa ujumla wake.

Kama vile mikataba ya biashara, aina zake, wanaostahili kuingia mikataba hiyo, biashara halali na haramu, usafirishaji wa bidhaa halikadhalika kupokea, kuharibika na kupotea kwa bidhaa.

Kutokana na kukua kwa biashara na kuongezeka kwa wimbi la uagizaji wa bidhaa kutoka nje au hata mkoa mmoja kwenda mwingine, makala hii itaeleza baadhi ya kanuni za kisheria kufuatia biashara ya kuagiza na kupokea mizigo ambayo ni muhimu mfanyabiashara na hata mlaji kuzingatia.

**KUBEBA HASARA**

La muhimu kujiuliza ni hili hivi hasara itabebwa na nani, mzigo ukipoteza au kuharibika wakati wa kusafirisha?

Kifungu cha 34( 2 ) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa ikiwa jukumu la kusafirisha mzigo au bidhaa ni la muuzaji, basi yeye ndiye atakayetakiwa kuingia mkataba wa usafirishaji mzigo kati yake na kampuni au anayetoa huduma ya usafirishaji.

Hivyo basi, ikiwa mzigo utapotea wakati ukiwa njiani au kuharibika kwa namna yoyote ile muuzaji ndiyo atakewajibika na upotevu au uharibifu na mnunuzi anaweza kukataaa kupokea mzigo uliharibika au kukubali kuupokea kwa sharti la kulipwa fidia.

Kama sehemu ya punguzo la thamani ya mzigo husika au ikiwa umepotea kabisa itabidi kurudishiwa hela yake/zake.

**MZIGO KUKATALIWA**

Kukataa kupokea mzigo au bidhaa ambayo haijatimia, ni jambo linalofafanuliwa na kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Uuzaji wa Bidhaa Tanzania kinatilia mkazo, ikiwa muuzaji atapeleka mzigo au bidhaa ambayo haijatimia basi mnunuzi anaweza kukataa kupokea mzigo huo.

Lakini ikiwa atakubali kupokea japo haujatimia basi atatakiwa kulipa pesa ile ile iliyo kwenye mkataba bila kukata au kupunguza hela kufidia bidhaa ambayo haijaletwa.

Kwahiyo ukikubali tu kupokea mzigo ambao haujatimia huwezi tena kusema napunguza na hela. Ukipokea tu sheria inasema unatakiwa kulipia hela yote mliyokuwa mmekubaliana. Hivyo basi kama hauko tayari kulipa hela yote basi lililo bora kwako ni kutopokea kabisa mzigo huo.

**ANGALIZO**

Kupokea bidhaa au mzigo uliozidi kunafafanuliwa na kifungu cha 32(2) cha Sheria hiyo kinachosema kuwa pale ambapo muuzaji atapeleka kwa mnunuzi mzigo ambao umezidi ile idadi waliyokubaliana kwenye mkataba basi mnunuzi anaweza kukataa kupokea mzigo wote au sehemu iliyozidi.

Lakini pia ikiwa atakubali kupokea mzigo wote basi atatakiwa kulipa pesa kwa kiwango kile kile walichokubaliana.

Hatakuwa na wajibu wa kuongeza pesa ati kwasababu mzigo nao umeongezeka. Hasara itakuwa kwa muuzaji aliyezidisha.

**BIDHAA KWA MAFUNGU**

Kupokea mzigo au bidhaa kwa mafungu au kwa awamu, ni suala la kutizama pia.

Kifungu cha 33 cha sheria hii kinaeleza kuwa kinakubali makubaliano ya kupokea bidhaa kwa mafungu au kwa awamu , lakini kimeweka msisitizo katika muda na malipo kufanyika kama makubaliano yalivyo Ikiwa bidhaa haitaletwa kwa muda uliokubaliwa basi mnunuzi anaweza kudai fidia au vinginevyo.

La muhimu ni kwamba makubaliano ya nani atabeba hatia au riski ni kwamba mara zote unapofanya biashara ambayo inahusisha kusafirisha mzigo iwe kwa barabara, treni, ndege au meli ni muhimu sana kukubaliana katika makubaliano yenu nani atabeba hatia ikiwa litatokea tatizo.

Hakikisha mnaandika kabisa kwenye makubaliano yenu kuwa kwa hatari yoyote au riski mhusika fulani ndiye atawajibika kulipia.

Kama ni bidhaa unaagiza kutoka nje angalia katika maelezo yao kama kuna habari ya bima au maelezo yanayoeleza nani mbeba hatia kama itatokea. Kama kifungu hicho hakipo ni wajibu wako kuwezesha kiwekwe.



## KALAMU YA MWALIMU

# Serikali iziongezee uwezo shule za kata

Na Reubeni Lumbagala

JUMA lililopita safu hii ilichapisha makala iliyokuwa na kichwa "serikali iziongezee uwezo shule za kata kitaaluma". Makala hiyo ilieleza namna ambavyo wanafunzi wa kidato cha sita wa shule za kata kwa mwaka huu 2019 walivyofanya vizuri katika matokeo ya kidato cha sita.

Aidha, hatua hiyo ilizinyanyua shule mbili za kata na kuzipeleka kwenye orodha ya shule 10 bora na shule nyingine 52 za kata ziliingia kwenye shule 100 bora kitaifa.

Hii ni heshima kubwa kwa serikali, walimu, wanafunzi na wazazi wenye watoto wanaosoma katika shule za kata kutokana na jamii kuwa na mtazamo hasi na kuzipuuza kuwa shule za kata si kitu nyingine zikibandikwa majina kama 'kayumba'.

Serikali imefanya kazi na juhudi kubwa za kutatua changamoto katika shule za kata, lakini pamoja na juhudi kubwa hizo bado changamoto kama vile; upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati, upungufu wa nyumba za walimu, mabweni, vyumba vya madarasa, madawati, matundu ya vyoo na uhaba wa vitabu vya kiada za ziada.

Changamoto hizi zimechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa sera ya Elimu Bila Malipo ambayo imeleta mwamko mkubwa kwa wazazi na walezi kupeleka watoto shule kutokana na serikali kubeba jukumu la kugharamia gharama za elimu kwa kupeleka fedha moja kwa moja katika akaunti za shule husika kila mwezi.

Kutokana na changamoto mbalimbali zinazozikabili shule za kata, Kalamu ya Mwalimu inatoa ushauri kwa serikali kuangalia namna ya kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi wa shule hizo kutokana na kazi nzuri wanazofanya.

Juhudi hizo zimezipaisha shule hizo hadi kupata mafanikio makubwa katika mitihani ya taifa hata kuzishinda baadhi ya shule za binafsi zenye ada kubwa.

Changamoto zilizopo katika shule za kata, kama zingetatuliwa ni dhahiri mafanikio makubwa zaidi yangepatikana katika matokeo ya mitihani ya taifa.

Hata hivyo, walimu na wanafunzi waliopo katika shule za kata hawajakata tamaa juu ya uwepo wa changamoto hizo bali kuongeza bidii katika kufundisha, kujisomea na kutafuta njia mbadala za kukabiliana na changamoto hizo ili kuweza kupata mafaniko katika taaluma.

Ni dhahiri wanafunzi wanaosoma shule za kata na wanaofanikiwa kupata daraja la kwanza katika mitihani ya taifa, walimu, mwanafunzi na wazazi wenyewe wanakuwa wamefanya kazi ya ziada kufikia mafanikio hayo kutokana na uwepo wa changamoto mbalimbali katika shule za kata na mazingira ya nyumbani ya baadhi ya wanafunzi wanaosoma shule za kutwa.

Hivyo basi, upo umuhimu wa serikali kuangalia namna ya kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi wa shule za kata kutokana na kufanya vizuri katika mitihani.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) wapitishe fungu maalum la motisha kwa walimu ambao masomo yao yamepata alama 'A'.

Aidha, fungu liwahusishe pia wanafunzi waliopata daraja la kwanza na kuwa wa uhakika wa kujiunga kidato cha tano na wengine kujiunga na vyuo vikuu.

Kwa kutoa motisha hiyo, itawaongezea walimu ari, nguvu na kasi ya kujituma zaidi katika ufundishaji na wanafunzi pia kujisomea kwa bidii ili kuweza kunufaika na motisha

**MOTISHA YA WALIMU.**

Serikali inaweza kutoa motisha ya fedha kwa walimu ambao wanafunzi wamepata 'A'. Hii itaongeza shauku kwa walimu kujituma zaidi katika ufundishaji. Pia serikali inaweza kutoa vyeti vya pongezi kwa walimu kama njia ya kutambua mchango wao ulioleta mafaniko katika mitihani ya taifa.

**KWA WANAFUNZI**

Serikali inaweza kutoa motisha kwa kuwanunulia wanafunzi zawadi kama madaftari makubwa watakayotumia wakiendelea na kidato cha tano na sita. Kadhalika kuwanunulia sare pia ni njia ya kuwapa motisha wanafunzi wanaofanya vizuri.

Vilevile, kupitia halmashauri wanazotoka wanafunzi waliopata daraja la kwanza, wanaweza kuwalipia ada ya mwaka mzima ya Shilingi 70,000 ili kuwasadia katika safari yao ya kujiunga kidato cha tano katika shule za serikali.

Kimsingi, motisha zikitolewa kwa wahusika, shule za kata zitaendelea kufanya vizuri na kuwafanya wanafunzi wafurahie kusoma katika sekondari hiyo.

Naendelea kuishauri serikali kama inavyowekeza katika kuzikarabati shule zake kongwe za sekondari pamoja na vyuo vya ualimu (TTC), kazi hiyo itakapomalizika, kazi ianze kwa shule za kata kwa kuzifanyia ukarabati na maboresho makubwa ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa kwa ustawi wa taaluma na maendeleo ya nchi. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: (+255) 764 666349**

# UTALII

# Tanzania yakamata

**Na Beatrice Philemon**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizo na vivutio vingi vya utalii ikiwa ni miongoni mwa nchi zinazoongoza barani Afrika.

Baada ya kuona umuhimu wa sekta hiyo katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kushirikiana na wadau wengine waliopo sekta ya utalii wameanza kuwekeza nguvu katika kutangaza vivutio vya utalii nchini China na Korea ya Kusini

Mambo kadhaa yanahusisha jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundo mbinu na kuhakikisha kuwa Tanzania inaongeza sehemu ya umiliki wa soko la utalii la China.

Vichocheo vikubwa vya maendeleo ya utalii hapa nchini ni pamoja na miundo mbinu ya uhakika na kwa mujibu wa TTB miundombinu hiyo ni viwanja vya ndege, barabara bora, hoteli za nyota tano, za nyota tatu, loji, mawasiliano ikiwamo mitandao na mikongo ya mawasiliano.

Yote haya ni ili mtalii anayehitaji kutembelea vivutio vya utalii aweze kufika kwa uraisi na kuwasiliana pia.

Ili Tanzania iweze kupata watalii wengi zaidi kutoka nchi ya China ikiwemo pia nchi ya Korea, TTB kwa kushirikiana na sekta binafsi na ya umma, imeanza kufanya ziara mbalimbali ili kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania katika miji ya Beijing, Shanghai, Chengdu, Guangzhou, Hong Kong, Nanjing na Changsha.

Jukumu hilo linahusisha safari za ndege za Air Tanzania zinazotarajiwa kuanza hivi karibuni kufika nchini China.

Akizungumzia mafanikio ya ziara ya utalii iliyofanyika Novemba mwaka 2018 na mwezi June mwaka huu, Mwenyekiti wa TTB Jaji Thomas Mihayo, anasema ziara hizi zimeanza kuzaa matunda kwa sababu Tanzania imeanza kupokea watalii na wawekezaji kutoka China.

"Mpaka sasa tayari tumeshapokea watalii zaidi ya 450 kutoka miji mbalimbali nchini China waliokuja kutembelea vivutio vya utalii wa Tanzania ikiwamo hifadhi ya Ngorongoro, Serengeti, maeneo ya mambo ya kale Bagamoyo, Zanzibar na pia kuangalia fursa za uwekezaji," anasema Mihayo.

Vile vile miongoni mwa matunda mengine katika ziara hizo ni kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya ushirikiano kati ya Bodi ya Utalii Tanzania na Kampuni ya Touchroad International Holdings Group yenye makao makuu katika jimbo la Shanghai, China.

Mkataba huo ni kwa ajili ya kuleta watalii 10,000 kutoka China hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

"Kupitia mkataba huu zaidi ya watalii 450 kutoka China wameishakuja Tanzania kwa ajili ya kutembelea vivutio vya utalii, anasema Mihayo.

**UTALII MAJIMBONI**

Akizungumzia ziara ya utangazaji utalii nchini China katika majimbo ya Beijing, Shanghai, Nanjing na Changsha iliyofanyika Juni mwaka huu, anasema kuwa lengo la ziara ilikuwa ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaongeza sehemu ya umiliki wa soko la utalii la China kwa kutangaza vivutio vya utalii vya taifa hili.

Aidha pamoja na utalii kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na safari mpya za ndege za ATCL kwenda China.

Katika ziara hizo TTB iliambatana na wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi ikiwamo Mamlaka ya Hifadhi Bonde la Ngorongoro, Wakala wa Huduma za Misitu (TES), Makumbusho ya Taifa, Idara ya Mambo ya Kale na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori.

Kwa Upande wa sekta binafsi kampuni 11 zilizoshiriki katika ziara hiyo ni pamoja na hoteli za nyota tano, kampuni za kupokea na kuongoza watalii.




Jaji Mihayo (kulia) katika moja ya mikutano ya kuzungumzia utalii wa Tanzania pam




Makala wa utalii, wafanyabiashara na waandishi wa habari katika Jimbo la Hong Kong nchini China wakimsikiliza Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Jaji Mihayo, akiwaelezea kuhusu vivutio vya utalii na fursa za uwezekaji zinazopatikana Tanzania. **PICHA: HISANI YA TTB.**

MAKALA

# WAPAA
# a soko China, Korea



oja naye ni Mkurugenzi wa TTB Utalii, Devota Mdachi. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

### MATOKEO

Akielezea matokeo ya ziara ya utangazaji utalii iliyoandaliwa na Bodi ya Utalii , kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania China Novemba, 2018, Jaji Mihayo, anasema kuwa ni matunda ya ziara hiyo.

Anaendelea kuonekana baada ya kampuni ya Paper Communications ya HongKong kuthibitisha kuwa italeta watalii 130 kutoka Hongkong .

Wakiwa nchini watatembelea baadhi ya vivutio vya utalii vya Ngorongoro Crater, Serengeti na vivutio vingine.

Aidha wakati wa ziara yao watalii hao, ambao baadhi yao 25 ni wafanyabiashara na wawekezaji, wataangalia pia fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

### MAONI YA BALOZI

Akieleza wakati wa hafla ya kuwakutanisha wajumbe kutoka Bodi ya Utalii na wawakilishi wa Kampuni ya Paper Communications iliyoandaliwa na Balozi wa Heshima wa Tanzania nchini Hongkong, Dk.Annie Wu alisema kuwa ziara ya kundi hilo la watalii 130 ni matokeo ya kazi ya utangazaji iliyoandaliwa na TTB mwaka jana.

Anasema wawekezaji hao walivutiwa sana na suala la amani na utulivu wa Tanzania pamoja na vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Wawakilishi wa Kampuni ya Paper Communications wanaeleza kwamba baadhi ya watalii hao wameonyesha shauku ya kutaka kuwekeza nchini na hivyo watatumia fursa ya ziara hii kuangalia maeneo ambayo wanaweza kuja kuwekeza.

### KUIKAMATA KOREA

Wakati huo huo, ujumbe kutoka TTB ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Jaji, Thomas Mihayo ulifanya ziara ya kutangaza utalii wa Tanzania mapema mwezi Julai 2019 katika nchi ya Korea Kusini.

Matokeo ya ziara hiyo iliyoandaliwa na Ubalozi wa Tanzania Nchini Korea Kusini, yamekuwa na mafanikio makubwa kutokana na mwitikio mkubwa waliopata kutoka kwa wadau wa utalii waliokutana nao, anasema Jaji Mihayo.

Ujumbe kutoka TTB ulikutana na wadau mbalimbali, wakuu wa utalii wa nchi hiyo akiwemo Byeong Sam Kim ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Wakala wa Utalii wa Korea Kusini (KTA).

"Katika kikao hicho, TTB na KTA tulikuwa na mazungumzo mahsusi yaliyolenga kuhamasisha suala la ushirikiano baina ya mawakala wa utalii wa Tanzania na Korea Kusini." Anasema.

Aidha, Kim anasema kuwa kwa mwaka 2018 idadi ya watalii milioni 26 kutoka Korea kusini walitembelea nchi mbalimbali duniani.

Anashauri kwamba ili TTB iweze kufanikiwa katika mikakati yake ya kulikamata soko la Korea Kusini ni muhimu kwa Tanzania kuwaunganisha wafanyabiashara ya utalii wa Tanzania na wenzao wa Korea Kusini.

Pia, anaonyesha utayari wake wa kushirikiana na TTB katika kufanikisha suala hilo na anaahidi kwamba kuongoza ujumbe wa mawakala wa utalii kutoka Korea ya kusini 20 watakaokuja nchini.

Wageni hao watafika katika ziara ya mafunzo itakayofanyika mwanzoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu.

Aidha, Kim alikubali kushiriki mwaliko uliotolewa na TTB wa kushiriki katika onyesho la kimataifa la Utalii la Swahili (Swahili International Tourism Expo). linaloandaliwa na TTB litakalofanyika Mlimani City kuanzia Oktoba 18 hadi 20 mwaka huu.

"Vile vile katika kuendeleza mikakati ya utangazaji utalii wa Tanzania katika masoko ya mashariki ya mbali, tulikwenda pia Korea Kusini ambako tulikutana na kufanya mazungumzo na baadhi ya kampuni za utalii zinazoongoza kwa kutoa watalii nje ya Korea Kusini na kuzihamasisha kuleta watalii wao nchini Tanzania." Anasema Mihayo.

Kampuni hizo ni pamoja na Kampuni ya Hanjin Travel na HanaTour za Seoul Korea Kusini.

Akieleza kilichojiri baada ya kukutana na mawakala hao, Jaji Mihayo anaeleza kwamba kampuni hizo zimekubali kuja Tanzania kuendeleza mazungumzo na TTB pamoja na kuangalia fursa za kuleta watalii wengi zaidi kutoka Korea ya Kusini nchini Tanzania.

Aidha, kampuni hizo zimekubali mwaliko wa kushiriki katika maonyesho ya utalii yanayoandaliwa na TTB ya Swahili International Tourism Expo -S!TE.

### UBIA NA ETHIOPIA

Wakati huohuo, ujumbe kutoka TTB pamoja na maofisa kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini waliweza kukutana na Rahel Gebre Meneja Mkuu wa Shirika la Ndege la Ethiopia nchini Korea ya Kusini.

Katika mkutano huo uliolenga kuweka mikakati ya ushirikiano kati ya TTB na ofisi ya Shirika la Ethiopia jijini Seoul katika kutangaza utalii wa Tanzania nchini Korea ya Kusini, hasa katika kurahisisha usafiri wa anga kwa watalii kutoka nchi hiyo.

Akizungumza baada ya Mkutano huo Balozi wa Tanzania nchini Korea Matilda Masuka anasema kwamba shirika hilo la ndege limekubali kushirikiana na ofisi yake pamoja na TTB katika kuandaa ziara ya mafunzo itakayofanyika Oktoba mwaka huu.

Shirika hilo litasaidia kutoa usafiri wa anga kwa mawakala wa utalii na waandishi wa habari watakaoshiriki katika ziara hiyo kwa makubaliano maalum.

Ujumbe kutoka TTB ilikutana na kampuni ya uwakala wa utalii ya Shoestring Travels ambayo imebobea katika utalii wa upandaji milima duniani.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo Youngbok Jang, alisema kampuni yake ipo tayari kushirikiana na TTB katika kutangaza Mlima Kilimanjaro na kuhamasisha watalii kutoka Korea kupanda mlima huo pamoja na kutangaza milima mingine ya Tanzania

Devota Mdachi Mkurugenzi Mwendeshaji wa TTB anasema kwamba soko la utalii la Korea ya Kusini ni moja ya masoko ya utalii yanayokua kwa kasi sana na kuwa jitihada zinaendelea kufanywa na TTB katika kukamata soko hilo.

"TTB imepanga mikakati madhubuti itakayoiwezesha Tanzania kuongeza idadi ya watalii kutoka nchi ya Korea ya Kusini," alisema Mdachi.

Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kutumia mitandao ya kijamii hasa Blog ya Naver ambayo asilimia 75 ya Wakorea hutembelea mtandao huo, kuandaa ziara za mawakala wa utalii , kualika baadhi ya vyombo vya habari vya Korea ya Kusini vyenye watazamaji wengi. Mwaliko huo unalenga kushiriki katika onyesho la utalii la Korea Tourism Fair na roadshow katika mji wa Seoul na Busan ,pia kutumia watu wenye ushawishi mkubwa.

Mdachi anasema kuwa kupitia ubalozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini TTB imeanza mipango ya kuandaa ziara maalum ya utangazaji utalii utakaofanyika Februari, 2020.

Pia kupitia ubalozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini wamepanga kuandaa ziara ya utangazaji mwakani ambayo itakutana pia na kampuni nyingine zaidi za Korea Kusini . Aidha, Mdachi anasema, TTB na ubalozi huo zitaalika mawakala pamoja na waandishi wa habari za utalii za nchi hiyo kushiriki katika onyesho la S!TE na kuhakikisha kwamba mawakala na waandishi hao wanatembezwa katika maeneo mbalimbali ya utalii nchini pamoja na kuonyeshwa fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii.



# MABUNGE SHULENI

## ■Mbinu inayonusuru mabinti mimba utotoni, yawajaza uthubutu, kujiamini, waiva kiuongozi

**Na Gaudensia Mngumi**

MARA nyingi imezoeleka kuwaona na kuwasikia watoto wa chini ya miaka 18 wakiimba na kutamba zaidi kwenye ngonjera na mashairi waliyokaririshwa ili kufikisha ujumbe mbele ya kusanyiko la viongozi wakiwamo wa kiserikali au wengine wanaojihusisha na maendeleo ya jamii au taaluma .

Ni kwa nadra, watoto hao wa shule za msingi wakiwa nje ya ngonjera na michezo ya kuigiza wanaweza wakaongea kwa kujiamini, kujitambua na tena bila woga wakatoa hoja zenye mashiko zinazowagusa wenye dhamana hadi kutoa maelekezo kushughulikia changamoto zinazoibuliwa na watoto hadharani.

Katika Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, Shule za Msingi Mnyahi , Namedi, Ruvuma na Mihambwe wanafunzi wamekuwa chachu ya mabadiliko kusimamia haki zao na kupinga ukatili dhidi ya watoto.

Aidha, mabinti wameimarika wakiwapinga wanaowadanganya na hadaa za ngono na kuwaachia mimba za utotoni.

Wasichana hao wanakataa kuozwa ndoa za utotoni na wanakumbusha wazazi na walezi kuwapa muda wa kusoma badala ya kuwatumikisha wakati wa jioni wakirejea nyumbani .

Wanataka nao kama walivyo wavulana wapewe muda ili watimize malengo yao ya elimu.

Ubavu wa kujiamini kutoa hoja za nguvu umefanikiwa kupitia kuanzishwa programu ya kuandaa bunge la wanafunzi.

Mabunge ya wanafunzi yanayofanana na kuongozwa kwa utaratibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yakisimamiwa na Spika na kujumuisha viongozi kama Waziri Mkuu, Katibu wa Bunge, mawaziri wa sheria, elimu, kazi pamoja wabunge.

Hivi karibuni timu ya wanahabari na maofisa wa shirika la Action Aid Tanzania (AATZ) ilizuru Shule ya Msingi Mnyahi, iliyoko wilayani Tandahimba mkoa wa Mtwara na kukutana na bunge la wanafunzi, ambalo pamoja na 'wabunge' kuonyesha uwezo mkubwa wa kujiamini, wanaeleza kuwa chombo hicho kimebadilisha fikra zao.

Wanasema wamepata ujasiri, kujiamini na wanaweza kuzungumzia hoja zao mahali popote na kuwasilisha changamoto pamoja na kuzifuatilia. Kama wanavyojieleza.

### KUBADILISHA MITIZAMO

Jukwaa hilo limekuwa chachu ya watoto kujifunza zaidi, spika wa bunge hilo Ajuaye Saidi, anasema. Binti huyu anatamba kuwa limemwezesha kujiamini, kuzungumza bila woga mbele ya hadhara, kujifunza masuala ya uongozi na siasa.

Aidha, katika kipindi kifupi anaweza kuongea na kuchambua masuala yanayomtinga msichana na mwanafunzi wa Tanzania.



Spika Ajuaye Saidi



Mbunge Mohamed Mitaji

Kama watoto wengine wa Mnyahi wabunge na spika wamejawa hamasa, ya kisiasa na wanafahamu kuhusu uchaguzi unaokuja wa serikali za mitaa na vijiji na baadhi wanaeleza kama wangepewa fursa wangegombea uongozi gani na kwanini ili kumaliza changamoto za watoto wa Tanzania.

### KUKATAA NGONO

Mbunge Hashuluna Hamimu wa darasa la saba, analitaja bunge hilo kuwa limewafunza mabinti kukataa vishawishi vya ngono na kuepuka magonjwa na mimba utotoni akisema:

"Pamoja na kuelimika kitaaluma, najua kujitunza kama msichana. Najiamini , nakataa hadaa za ngono, sijihusishi na wanaume na hata nikipewa hela nawaambia niacheni nisome."

Binti huyu anasema wasichana shuleni hasa wa darasa la saba wanawaambia wazazi waache kuwatumikisha wakirudi nyumbani. Wanawahimiza wawape muda wa kusoma, iwapo wazazi wanawakataza wasichana kwenda shuleni wanaripoti kwenye uongozi wa shule na kijiji .

Aidha, anasema wana uwezo wa kupaza sauti na kupinga ukatili unaofanywa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa walimu na viongozi.

Mbunge mwingine ni mwanafunzi Mohamed Mitaji, akiwa wa darasa , pamoja na kuuliza maswali kwa ufasaha kuhusu sababu za kesi za mimba za utotoni kumalizwa kimya na wazazi nyumbani wakati wa kikao cha bunge hilo, anasema :

"Ninafahamu haki za watoto, ninaweza kujieleza zaidi ndani ya jamii, nasimama na kumuuliza kiongozi yeyote swali pale ninapopewa nafasi."

### LENGO LA MABUNGE

Mabunge hayo yaliyoanza mwaka 2010 katika shule za msingi za Wilaya za Newala na Tandahimba, yalianzishwa na Shirika la Action Aid Tanzania (AAT). Katika ziara hiyo kwenye wilaya hizo, Mratibu wa AAT Tandahimba na Newala mkoani Mtwara, Dinno Celestine, anasema mabunge yalianzishwa kwa lengo la kuwajengea watoto uwezo wa kujiamini ,kujitambua pia kuwapa jukwaa la kuzungumzia na kudai haki zao kama kupinga ukatili, unyanyasaji na kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kwa mabinti.

Anasema kupitia jukwaa la bunge la wanafunzi lenye wabunge na mawaziri wakike na wakiume, sauti za watoto hao zinapazwa na kufikisha ujumbe kwenye mabaraza ya madiwani, viongozi wa wilaya, mikoa na pia husikika kwenye vyombo vya habari ikiwa ni njia ya kubainisha na kuondoa changamoto zinazowaumiza na kuwakwamisha watoto hao.

Akizungumza katika ziara hiyo, Celestine anaeleza kuwa wabunge hao walishiriki kwenye Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kiwilaya na kuelezea changamoto za watoto mbele ya viongozi wakiwamo madiwani, viongozi wa wilaya na wadau wa asasi mbalimbali.

Kadhalika, hoja zao zilirushwa sehemu mbalimbali nchini kupitia vyombo vya habari na baadhi ya runinga kama ITV ilirusha bunge hilo kwenye kipindi cha watoto.

Mratibu wa AATZ Tandahimba na Newala, anasema wangependa sauti za wabunge hao zisikike zaidi ili waweze kufikisha ujumbe mbele ya viongozi wenye dhamana kwa lengo la kuboresha maisha ya mtoto.

Mabunge ya wanafunzi kwa mujibu wa Mratibu huyo, awali yalikuwa klabu zilizoanzishwa mathalani kulinda mazingira au kusimamia afya shuleni, baada ya kubadilishwa na kuboreshwa yamefanikisha kukemea mimba na ndoa za utotoni.

Anataja kuwa watoto kujiamini na kujisimamia kikamilifu, kujitetea na kutaka kuwe na mabadiliko ambayo yamejitokeza kwenye maeneo mengi kwenye mabunge hayo ni moja ya mafanikio ya kujivunia.

### MIMBA KUPUNGUA

Katika ziara hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii na Mratibu wa Dawati la Jinsia wa Wilaya ya Tandahimba, Neema Shungu, katika mahojiano kuhusu suala la mimba, anakiri kuwa hamasa miongoni mwa mabinti na wanafunzi imepunguza tatizo hilo.

Anasema mimba za wanafunzi shuleni zilipungua akitaja takwimu za 2018 kuwa zilikuwa mimba 54 na kwamba mwaka huu kuanzia Januari mpaka Agosti zimepatikana mimba tisa.

Licha ya kwamba hakufafanua zaidi takwimu hizo kwa upande wa sekondari na shule za msingi anasema kuwahamasisha wasichana kudai haki na kupinga ukatili kumebadilisha hali.

### AJIRA ZA WATOTO

Mhamasishaji maendeleo (CDF), anayeshirikiana na AATZ kuandaa bunge la wanafunzi katika shule za Namedi na Mnyahi, Mohamedi Lulanje, anasema mabunge hayo yamebadilisha mitizamo ya wanafunzi.

Lulanje anasema wamefunzwa na kupata utambuzi mkubwa kwenye kudhibiti ajira za watoto na sasa si rahisi kuwatoa watoto vijijini ili kuwatumikisha majumbani kama ilivyokuwa hapo awali.

Anasema ni kwa sababu wanazungumza, kufuatilia na kufikisha taarifa zinazohusu masuala ya haki, maendeleo na ulinzi wa watoto wakiwamo mabinti.

Lulanje anaeleza kuwa kwa kushirikiana na AATZ na walimu wanawaandaa wanafunzi na wabunge katika mada mbalimbali kama kupinga ajira za watoto, kufahamu sheria zinazowalinda, matatizo yanayowakwamisha kusoma, usawa wa kijinsia na kupinga ukatili dhidi ya watoto na wasichana.

### JUKWAA LA VIONGOZI

Walimu wa Shule ya Mnyahi wanaamini kuwa bunge la watoto ni kichocheo kwa wanafunzi kufahamu haki za msingi , kujengewa uwezo wa kuuliza maswali na kuhoji masuala ya msingi.

Wanaeleza kuwa wabunge wanaalikwa sehemu mbalimbali kutoa ujumbe kupitia bunge hilo, wanafunzi wengi wanahamasika kufuatilia masuala ya kisiasa, uchumi na kutamani kusoma zaidi ili kuwa viongozi.

### MAPENDEKEZO

Kwa ujumla walimu na wahamasisha maendeleo wanashauri serikali kusaidia ili kuwa na mabunge ya wanafunzi endelevu.

Wangependa warekodiwe ili mijadala itumike kwenye runinga na mabunge haya yaanzishwe nchi nzima kama zilivyo programu za michezo ya shule za msingi Umitashumta yote haya ni kuwasaidia na kuwajengea uwezo wanafunzi wakiwamo wanaoishi vijijini.

HABARI KIMATAIFA

# Hukumu mlanguzi dawa za kulevya yaiva Marekani

**NEW YORK, Marekani**

HUKUMU ya anayetajwa kuwa mlanguzi mkubwa wa dawa za kulevya, Baktash Akasha, ilitarajiwa kutolewa jana jijini New York nchini Marekani.

Akasha na nduguye Ibrahim walikamatwa mjini Mombasa mwaka 2014 wakiwa pamoja na raia kutoka mataifa ya Pakistani na India.

Ndugu hao wa Akasha wanatuhumiwa kutumia ghasia, mauaji na kutoa rushwa kulinda biashara yao.

Wanatuhumiwa kupanga mauaji ya raia wa Afrika kusini anayefahamika kwa jina moja pekee la 'Pinky'.

Hukumu hiyo ilitarajiwa kutolewa jana na taarifa zilieleza kuwa ofisa wa zamani katika idara ya upelelezi nchini humo (DCI), majaji kadhaa na maofisa wengine wa serikali huenda wakahamishwa kupelekwa Marekani kukabiliwa na mashtaka yanayohusu ulanguzi wa dawa za kulevya.

Gazeti la Nation nchini Kenya linaripoti kuwa duru ziliarifu kwamba serikali ya Marekani tayari imeifahamisha Kenya kuhusu nia hiyo ya kuwashtaki washukiwa katika mahakama za Marekani.

Hatua inayomaanisha kwamba huenda katika siku zijazo kukashuhudiwa kuwasilishwa kwa washukiwa kwa maofisa wa usalama wa Marekani.

Mji wa Mombasa nchini Kenya unapitia madhara mengi ya dawa za kulevya, huku familia hiyo ya Akasha ikilaumiwa kuchangia janga hilo kwa kiasi kikubwa.

Mwandishi kutoka eneo hilo, Francis Ontomwa, alieleza kwamba unapolitaja jina la Akasha mjini Mombasa, linaibua woga na wasiwasi mwingi.

Kwa miaka kadhaa, familia ya Akasha iliendesha na kujenga himaya ya ulanguzi wa mihadarati kutoka kitovu cha mji huo wa Mombasa, kuunganishwa na Afghanistan, Ulaya na hata nchini Marekani.

Madhara ya biashara hiyo yanaonekana wazi katika mji huo wa pwani ya Kenya, kwa mfano Salma Hemed ni mwanaharakati wa kutetea haki za binadamu kutoka Shirika la Haki Afrika ambalo limekuwa likijishughulisha na harakati za kupambana na madhara ya biashara hiyo haramu miongoni mwa vijana.

"Kwa wale wenye kuuza wanahitaji vijana wa kutoka nyanja tofuati. Na katika kuonja mihadarati, inawafanya wao waanze kuwa watumiaji wakuu na pia kuitegemea hadi kuwa waraibu na kuanza kuwa watumiaji wakuu wa mihadarati". Alisema Salma.

***BBC***



Waziri Mkuu mpya wa Sudan, Abdalla Hamdok. **PICHA: MTANDAO**

# Upinzani huko Zimbabwe waahirisha maandamano

**HARARE, Zimbabwe**

UPINZANI nchini Zimbabwe umeahirisha maandamano yaliopangwa kufanyika jana baada ya kuapa kuendelea kukaidi marufuku ya polisi dhidi ya maandamano ya kupinga Serikali.

Tendai Biti kutoka chama kikuu cha upinzani nchini humo MDC aliithibitishia BBC kwamba maandamano hayo hayatofanyika kama ilivyopangwa awali. Alieleza kuwa uamuzi huo umeondoshwa mikononi mwao na maofisa wa polisi waliozifunga barabara zinazoelekea mjini.

Mahakama nchini humo ilitupilia mbali ombi la MDC kutaka marufuku hiyo ya polisi ifutiliwe mbali.Mamia ya waandamanaji kadhaa waliokusanyika kukaidi marufuku hiyo, walitawanywa. Aidha, kuna maofisa wengi wa polisi wanaopiga doria katika eneo la mjini.

Awali kundi hilo la upinzani Zimbabwe' liliapa kwamba lingeendelea kuandaa maandamano katika mji mkuu Harare na kukaidi marufuku ya polisi. Chama cha MDC kiliitisha maandamano hayo ya umma kulalamika namna serikali inavyoshughulikia uchumi wa nchi hiyo.

Takriban raia 5,000,000 wa Zimbabwe wanahitaji msaada kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN). Chama cha MDC kilisema kimewahakikishia maofisa wa utawala kwamba maandamano hayo yangekuwa ya amani.

Hata hivyo, polisi walisema wana ushahidi kwamba maandamano hayo yaliyopangwa yangekumbwa na ghasia.

"Ilani ya zuio" inayopiga marufuku maandamano hayo ilitolewa na maofisa mjini Harare," alisema msemaji wa polisi Paul Nyathi.

Katika kuijibu kauli hiyo, ofisa wa MDC aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba chama hicho hakifahamu kuhusu zuio lolote na kwamba maandamano yataendelea kama yalivyopangwa.

"Maisha nchini Zimbabwe leo ni mabaya kuliko yalivyokuwa chini ya utawala wa Robert Mugabe," mwanasiasa wa MDC Fadzayi Mahere aliiambia BBC.

Polisi walitawanywa hadi katika makao makuu ya chama cha MDC na watu wamelisusia eneo la mjini, huku maduka yakiwa yamefungwa kinyume n ailivyo kawaida anaeleza mwandishi wa BBC Shingai Nyoka mjini Harare.

Haya yote yanajiri baada ya takriban wafuasi sita wa mashirika ya kiraia na wa upinzani kudaiwa kutekwa na kuteswa mapema wiki hii. Shirika la kutetea haki za binaadamu Zimbabwe lilisema waathiriwa walituhumiwa kushinikiza watu kuandamana. BBC.

## Waziri Mkuu wa Sudan kuthibitishwa Jumanne

**KHARTOUM, Sudan**

WAZIRI Mkuu mpya wa Sudan atatangazwa hivi karibuni. Jina lake limepitishwa juzi Alhamisi Agosti 15 na wawakilishi wa waandamanaji ambao walitakiwa kutoa jina la mtu atakayeshikilia nafasi hiyo.

Waziri huyo mkuu mpya wa Sudan anayeitwa Abdalla Hamdok atathibitishwa Jumanne, Agosti 20 na Baraza Kuu la Uongozi wa Sudan , ambalo ni taasisi mpya la mpito.

Abdalla Hamdok, ambaye ni mchumi mbobezi alikuwa anashikilia wadhifa wa Naibu Katibu wa Tume ya Uchumi ya Afrika katika Umoja wa Mataifa hadi mwaka jana.

Aliteuliwa bila kupingwa Alhamisi iliyopita nchini humo kuongoza serikali ya mpito ijayo ya Sudani.

Serikali ambayo raia watakuwa na nafasi muhimu kwani wananchi watapewa wizara 18 kuziongoza ilhali jeshi litakuwa na wizara mbili tu ya Ulinzi na ya Mambo ya Ndani.

Uchaguzi wa Abdallah Hamdok unatarajiwa kupitishwa rasmi Jumanne ya wiki ijayo. Uamuzi wa mwisho utatoka kwa Baraza Kuu, ambalo litaongoza katika kipindi chote cha mpito cha nchi hiyo.

Taasisi hiyo inatarajiwa kuundwa kesho Jumapili Agosti 18, siku moja baada ya hafla ya kutiwa saini kwa makubaliano ya jumla yanayoweka masharti ya kipindi cha mpito na kugawana madaraka kati ya raia na jeshi.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika wiki za hivi karibuni baada ya miezi nane ya mvutano na machafuko ambayo yalisababisha vifo na kupoteza maisha ya watu zaidi ya 250 waliokuwa waandamanaji.

Makubaliano hayo pia yanatoa nafasi ya kuundwa kwa "Kamati ya Uchunguzi Huru" ili wahusika wa vitendo hivyo wawajibishwe.

Wakati huo huo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani imeweka vikwazo dhidi ya Salah Gosh, Mkuu wa Idara ya Ujasusi wakati wa utawala wa Omar Hassa al-Bashir kwa "kuhusika katika ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu nchini Sudani."

Taarifa hiyo ilitolewa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, Jumatano wiki hii ikisema Salah Gosh alikuwa mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa (NISS), idara ya ujasusi ya Sudani katika utawala wa Omar al-Bashir.

**RFI**

# HADITHI


# Jumba Jekundu-14

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawatajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Japo ilikuwa usiku, lakini Kadili alishuhudia uzuri wa jumba hilo ambalo anaingizwa ndani yake huku akiwa hajui kama atatoka ndani ya jumba hilo jekundu hai, amekufa, au hatotoka milele kwa kuuawa na kuzikwa humo humo.

Wakati akiwa kwenye mawazo hayo, ghafla mlango ulifunguliwa. Aliingia baunsa mmoja ambaye hakuwa miongoni mwa wale walioukuja nyumbani kwao.

Kilichomtisha ni kwamba aliingia na mkanda wa suruali ambao unaonekana kabisa kuwa kazi yake ilikuwa ni moja tu kumpigia mtu.

Mtu mwenyewe ni yeye. Baunsa alifunga mlango. Ndani kulikuwa na balbu moja iliyokuwa inawaka na kutoa mwanga hafifu.

"Kijana kwa kawaida mimi huwa sipendi kupiga, kuumiza au kuua watu." Baunsa alianza kujinadi, huku Kadili akiwa hajui kama maneno yake ni swali, maelezo au onyo, lakini ilijikuta akiitikia "ndiyo".

"Sasa mimi hapa nataka unijibu maswali yangu machache tu nitakayokuuliza. Ukinijibu kiufasaha na ukweli, nitakuachia na hapa utaondoka kwenda kuungana na familia yako. Lakini kama ukinijibu utumbo, utapata mkong'oto ambao hujawahi kuushuhudia maishani mwako. Pia humu hutoondoka. Utauawa na kuzikwa humu humu ndani."

Mkanda wa suruali alioushika na mkwara aliotoa, ulimfanya Kadili ahisi shari. Hakujua ni maswali gani ambayo baunsa huyo anataka kumuuliza. Na vipi kama akijibu vile ambavyo jamaa huyo hataki ajibu?

Hakujua kama amwambie 'uliza' au la. "Nisikilize kwa makini." Sauti nzito yenye mikwaruzo ilipenya tena masikioni mwa Kadili.

"Edina ukoje naye?" Ni swali ambalo hakutegemea kabisa kuulizwa kwa wakati ule.

Na hapo hapo ndipo alipogundua kuwa kuchukuliwa kwake nyumbani kulitokana na sababu ya mrembo Edina na si kitu kingine.

Alikumbuka tahadhari aliyopewa na baunsa huyo kuwa akijibu ndivyo sivyo basi atakiona cha moto.

'Edina yupi?" Alijikuta tu naye akiuliza swali. "Kumbe wewe jeuri siyo?" Yalikuwa ni maneno ambayo sekunde chache baadaye yalifuatiwa na vitendo.

Mkanda ulitua mgongoni kwa nguvu kubwa. Akahisi uchungu ambao hakupata kuusikia hata siku moja. Alitaka apige kelele za "mamaaa", lakini sauti haukutoka.

Alijinyonganyonga na kugugumia kwa maumivu makali. "Narudia tena, Edina ukoje naye?"

"Ni rafiki yangu tu." Alijibu kwa tabu na mateso makali yaliyotokana na maumivu.

"Rafiki yako kivipi?"

"Nilikutana naye kwenye disco, yeye akaniomba nicheze naye, akawa amenizoea, kila anapokuja blue star, akinikuta, tunasalimiana na anataka tucheze naye. Ni hivyo tu bwana mkubwa."

"Hata macho yako yanaonyesha kuwa wewe ni muongo." Baunsa alionyesha kutokubaliana na jibu lile.

"Ni kweli, ni hivyo tu hakuna kingine bwana mkubwa." Alijibu katika namna ambayo ilionyesha kama kuomba msamaha.

"Na kama hivyo ilikuwa ni kosa, basi naomba nisamehewe, sitorudia tena." Kadili alizidi kujitetea.

"Wewe una uhusiano wa kimapenzi na Edina, si ndiyo?" Ilikuwa ni tuhuma lilioambatana na swali.

"Hapana bwana mkubwa, mimi siwezi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke kama Edina."

"Kwa nini?"

"Edina ni mwanamke wa kitajiri na mimi masikini, haiwezekani, ilikuwa ni kucheza tu muziki." Kadili alizidi kusisitiza na kusihi huku akiwa na woga kwani alijua muda wowote ule anaweza kuongezewa kichapo.

"Utachezaje muziki na mwanamke wa mtu?"

"Bwana mkubwa mimi sikujua hilo, hakuna hata siku moja ambayo aliniambia kuwa ni mke wa mtu..."

"Kwa hiyo ukaamua kumchukua wewe." Baunsa alimkatisha.

"Hapana, mimi siyo demu wangu, nilikuwa nacheza naye tu, halafu hatujawahi kukaa hata dakika tano kuongea naye. Kuna siku tu yeye aliniuliza jina na yeye akaniambia jina lake na anakokaa na mimi nikamwambia ninakoishi, basi hatujawahi kuongea kingine zaidi ya hicho."

Baunsa aliahirisha maswali kwa muda. Akawa kama kuna kitu anafikiri.

"Haya unayoniambia kama ni kweli nitajua na kama unaniongopea pia nitajua." Aliongea kwa sauti kama ya kunong'oneza na akageuka, akafungua mlango na kutoka, akimuacha Kadili akiendelea kukaa selo.

****************************
*************

> **"Hapana, mimi siyo demu wangu, nilikuwa nacheza naye tu, halafu hatujawahi kukaa hata dakika tano kuongea naye. Kuna siku tu yeye aliniuliza jina na yeye akaniambia jina lake na anakokaa na mimi nikamwambia ninakoishi, basi hatujawahi kuongea kingine zaidi ya hicho."**

Tayari kulikuwa kumepambazuka, mlango ulifunguliwa. Macho ya Kadili yalikutana na kipande kingine cha mtu. Mweusi na mwenye nywele nyingi.

Aliingia na kumwinua Kadili. Alitii amri ya mtu huyo. Hakuongea kitu chochote. Alimtoa nje ya nyumba na kumpeleka nyuma ya jumba hilo kubwa.

Kadili alizidi kushangaa uzuri wa jumba hilo lenye rangi nyekundu tupu, lakini iliyopambwa kwa nakshi na ufundi wa hali ya juu.

Nyumba ya jumba hilo kulikuwa na bustani yenye maua, miti na majani yaliyopambwa kwa ustadi na kuvutia macho cha kiumbe chochote kitakachofika hapo.

Kadili alishangaa uzuri ya maua ya rangi mbalimbali kana kwamba ni paradiso. Hata hivyo hakujua safari ile ilikuwa inaishia wapi.

Kwa sababu alikuwa mateka, alitii chochote kile ambacho anatakiwa kufanya.

Safari iliishia pembezoni kidogo mwa bustani hiyo. Kulikuwa na matuta machache ambayo yalionekana hayakufukiwa vema.

Mtu yule alisimama kwa sekunde kadhaa na kuyatazama, kana kwamba anaona kwa mara ya kwanza.

"Unajua kuna nini hapa?" Sauti ya mtu yule ambaye yeye hakuonekana baunsa kama wenzake, ila unene ule ni umbile lake la asili.

"Hapana."

"Haya ni makaburi." Alinyamaza kwanza na kuangalia Kadili kana kwamba alitaka kuyasoma mawazo yake, mara baada ya kupokea taarifa hiyo.

Miguu ilianza kumtetemeka.

"Sasa mimi hapa nataka unijibu maswali yangu machache tu nitakayokuuliza. Ukinijibu kiufasaha na ukweli, nitakuachia na hapa utaondoka kwenda kuungana na familia yako. Lakini kama ukinijibu utumbo, utapata mkong'oto ambao hujawahi kuushuhudia maishani mwako. Pia humu hutoondoka. Utauawa na kuzikwa humu humu ndani."

Akayakumbuka maongezi hayo aliyoyafanya masaa kadhaa yaliyopita na yule jamaa baunsa. Ndipo alipojua kuwa akifanya masihara huenda akauawa na kuzikwa ndani ya jumba hilo jekundu.

Sasa alitambua kuwa lengo la kuletwa pale ni kuonyeshwa makaburi ya watu wengine waliowahi kuingizwa kwenye jumba hilo.

"Makaburi haya wamezikwa watu ambao jeuri. Waliokuwa wanajifanya wajanja na hawataki kujibu ukweli maswali waliyoulizwa.

Sasa na wewe kama unataka uzikwe humu, jifanye mjanja. Inabidi ujibu maswali yote kwa ufasaha na ukweli." Alisema huku mkono ukimshika tena Kadili baada ya kuachia kwa sekunde kadhaa.

"Tena hawa wote wanazikwa wakiwa hai. Wanafia humo humo kaburini. Mimi nilitaka kukuonyesha tu, kwa hiyo yule jamaa akija tena kukuuliza maswali yake, usimdanganye, mjibu sahihi, umesikia?"

Kadili hakujibu kitu. Hakujua sasa ni jibu gani ambalo walitaka kutoka kwake. Ana uhakika kuwa alijibu maswali yote kwa ufasaha, na hakuongopa hata chembe.

Aseme ni kweli ana mahusiano na Edina wakati si kweli? Na kama akijibu hivyo ndiyo itakuwa salama yake kutoka ndani ya jumba jukundu akiwa hai? Aliwaza.

*Itaendelea Jumamosi*



# POCHETTINO
## HATISHWI NA WANAOSEPA SPURS

**LONDON, England**

MAURICIO Pochettino amesema kwamba hali ya mikataba kwa wachezaji wake wa kikosi cha Tottenham hakutaathiri upangaji wa kikosi kwenye michezo ya Ligi kuu kwa mujibu wa Gazeti la Evening Standard.

Christian Eriksen, Toby Alderweireld na Jan Vertonghen wote wapo kwenye mwaka wao wa mwisho wa mikataba yao ya sasa, huku majaliwa yao yakiwa hayajulikani.

Huku dirisha la usajili la Ulaya likikaribia kufungwa kwa wiki chache zijazo, Spurs wanaweza kuwauza wachezaji wake ambao wanaonekana kutaka kuondoka klabuni hapo.

Danny Rose, ambaye amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake, aliambiwa atafute sehemu ya kwenda kabla ya Spurs kwenda kwenye msimu wa maandalizi ya msimu mpya barani Asia.

Hata hivyo, licha ya hali hiyo, Pochettino amesisitiza kwamba ataendelea kuchagua kikosi chake bila kuangalia hali ya mikataba ya wachezaji ndani ya kikosi hicho.

Eriksen alianzia benchi kwenye mchezo wa ushindi wa Spurs wa mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa kabla ya kupewa nafasi kipindi cha pili.

# STERLING AFANANISHWA NA MESSI, RONALDO

**MANCHESTER, England**

HUKU akiwa amefunga mabao 17 msimu uliopita, matatu katika mechi moja msimu huu, Raheem Sterling yuko tayari kwa msimu mwingine bora mwaka huu na anatajwa kwamba anaweza kuwa kwenye anga moja na kina Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Mshambuliaji huyo wa Man City alikuwa na kampeni ya kipekee 2018-19 , akichaguliwa na waandishi kuwa mchezaji bora, mchezaji mwenye umri mdogo wa mwaka pamoja na kushirikishwa katika timu bora ya mwaka baada ya mabao yake kuisaidia timu yake kushinda taji la Ligi Kuu katika msimu wa pili mfululizo ambao pia waliweza kushinda mataji matatu.

Pia amekuwa mchezaji muhimu katika kikosi cha Gareth Southgate akitajwa kuwa mchezaji maalum na mkufunzi wake Pep Guardiola na akiwa na umri wa miaka 24, miaka yake bora iko siku zijazo.

Katika kipindi cha BBC Radio 5 Jumatatu usiku - swali liliulizwa iwapo Sterling anaweza kuwa na msimu kama ule wa Messi - mshindi mara tano wa taji la Ballon d'Or na mfungaji mabao 30 na zaidi kila msimu ambaye kila mtu anaweza kujivunia.

Sterling alifunga mabao 25 katika mashindano yote msimu uliopita yakiwa ndio mabao mengi aliyowahi kufunga katika msimu mmoja na aliendeleza msururu huo wa mabao kwa kufunga hat-trick katika mechi ambayo City iliibuka mshindi kwa mabao matano wakicheza dhidi ya West Ham Jumamosi.

Akiwa na umri wa miaka 24 na siku 245 - Sterling alicheza na kutoa mchango kama ule wa Messi wakati mshambuliaji huyo wa Argentina alipokuwa na umri kama huo.

Tofauti iliyopo kuhusu kiwango cha usaidizi wa kila mchezaji alichochangia katika wakati huo si kubwa - 90 kwa Messi ikilinganishwa na Sterling aliyekuwa na 68 - lakini ni ufungaji wa mabao mengi wa Messi ambao unamfanya kuwa mchezaji wa kipekee.

Huku Sterling akijishusha kwa kufunga mabao 25 msimu uliopita, machache yaliofungwa na Mesi katika misimu yake 11 ni mabao 38.

Kwa Sterling kulinganishwa na Messi atalazimika kuongeza kiwango chake cha mabao maradufu.

"Raheem anaendelea kuimarika," alisema aliyekuwa mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Ian Wright akizungumza na BBC Radio 5 Live.

"Ni hodari sana jinsi anavyocheza na na kutamba na mpira na ufungaji wake ni mzuri zaidi. Ni rahisi kumuona mtu kama Raheem akimaliza na mabao kati ya 35 - 40 msimu huu kutokana na jinsi anavyocheza , fursa zinazotengenezwa na Man City na jinsi anavyofunga mabao."

Thamani yake ilitokana na shinikizo nyingi kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 20 na pengine haishangazi ni kwa nini Sterling hakuweza kuonyesha mchango wake alipotaka kutoa.

Msimu wa 2016, wakati Sterling alipokuwa na msimu mbaya wa Ulaya ambapo alitolewa baada ya kipindi cha kwanza akiichezea England dhidi ya Wales kufuatia kipindi kibaya cha kwanza, alipokea ujumbe katika simu yake uliosema: "Usijali najua wewe ni mchezaji mzuri, Utakaponifanyia kazi, nitakupigania."

## NEVILLE AIPA UBINGWA UNITED KABLA YA LIVER

**LONDON, England**

NYOTA wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Gary Neville amesema kwamba Manchester United itatangulia kubeba ubingwa wa Ligi Kuu England kabla ya Liverpool kufanya hivyo.

Msimu uliopita, Man United ya kocha Ole Gunnar Solskjaer ilimaliza msimu ikiwa imeachwa pointi 31 na Liverpool, waliomaliza nafasi ya pili na kushindwa pointi moja tu na Manchester City iliyobeba ubingwa wa Ligi Kuu England, lakini Neville bado anawapiga kijembe mahasimu wao hao.

Wakati msimu huu, Liverpool wakiaminika kwamba wataendelea kuchuana na Man City kwenye mbio za ubingwa, lakini Neville anaamini kwamba wakali hao wa Anfield wataendelea kusubiri na Man United watabeba ubingwa huo kabla yao.

Liverpool haijabeba ubingwa wa ligi tangu mwaka 1990 na haijanyakua ubingwa wa Ligi Kuu England tangu ilipoanza kuitwa Premier League, huku Man United wenyewe wakiwa hawajabeba ubingwa huo tangu Sir Alex Ferguson alipostaafu mwaka 2013.

Neville alisema: "Ninaweza kuwahakikishia hilo, Manchester United watashinda ubingwa wa Ligi Kuu England kabla ya Liverpool, hilo ndilo ninaloliona. Sina maana kwamba nawakosea heshima Liverpool, lakini ndilo ninaloliona Man United watakuwa mabingwa kabla ya Liverpool."

Beki wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher ameamua kumjibu Neville kwa kudai kwamba Liverpool watabeba ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya Man United.

Man United waliichapa Chelsea 4-0 kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu England, wakati Liverpool wao walishinda 4-1 dhidi ya Norwich City kwenye mchakamchaka wa ligi hiyo ulioanza wikiendi iliyopita.

HABARI MICHEZO



# ANDY RUIZ

## AKATAA KUPIGANA NA JOSHUA SAUDI ARABIA

**NEW YORK, Marekani**

BONDIA bingwa anayeshikilia mataji matatu katika uzito wa juu, Andy Ruiz Jr, amesema hajatia saini mkataba wa kupigana na Anthony Joshua nchini Saudia na anaamini pambano hilo litafanyika New York.

Pambano hilo la marudiano lililopangwa kufanyika Desemba 7, mwaka huu nchini Saudia lilitangazwa Ijumaa na promota wa Joshua, Eddie Hearn.

Ruiz hakuzungumzia kuhusu pambano hilo ama hata kuchapisha katika mitandao ya kijamii hadi siku ya Jumatano.

Bondia huyo mwenye umri wa miaka 29, aliiambia ESPN FC nchini Mexico: "Sijatia saini makubaliano yoyote kufikia sasa kwa sababu bado tunaendelea kujadiliana."

Alipoulizwa kuhusu pambano hilo kufanyika Saudia alisema: "Wanataka kuliandaa huko, lakini lazima tuone pale tutakapojadiliana na timu yangu. Ningependa pambano hilo kufanyika tena New York."

Ruiz alimshinda Joshua ambaye alikuwa anapigiwa upatu kushinda pambano hilo kwa urahisi katika ukumbi wa Madison Square Garden mjini New York Juni Mosi, mwaka huu.

Baada ya kupata ushindi alichukua mataji ya IBF, WBA na WBO na kuwa raia wa kwanza wa Mexico kushinda mataji hayo katika uzito wa juu duniani.

Joshua alitumia haki yake ya kutaka pambano la marudiano na promota Hearn amesisitiza kuwa Ruiz ni sharti atie saini makubaliano hayo kwa kuwa ni miongoni mwa mkataba wa pambano lao la kwanza.

Hearn amesema kuwa timu ya Joshua inafaa kumjuza Ruiz wakati, tarehe na ukumbi wa pambano hilo na kwamba huenda bingwa huyo akakabiliwa kisheria iwapo mpambano huo hautafanyika.

Waandalizi wa pambano hilo nchini Saudia wamewekeza kitita cha dola 40 kuliandaa, lakini kumekuwa na ukosoaji mkubwa wa kulipeleka eneo kama hilo ambalo linadaiwa kuwa na rekodi mbaya ya haki za kibinadamu.

Shirika la Amnesty International limesema kuwa hatua hiyo inatoa fursa kwa mamlaka ya Saudia kusafisha rekodi yake mbaya kupitia michezo.

# Semenya: Wananiogopa kwa sababu hawaniwezi

**CAPETOWN, Afrika Kusini**

MSHINDI mara mbili wa riadha wa Olimpiki, Caster Semenya, amesema "hajawahi kuhisi kuungwa mkono" na wanawake wengine kwenye michezo.

Mshindi huyo mara tatu wa mbio za mita 800 hatatetea taji lake mjini Doha Septemba mwaka huu baada ya kugonga mwamba mahakamani kuhusu kutumia dawa za kupunguza homoni za testosterone kwa wanariadha wa kike.

"Wananilenga kwa sababu hawaniwezi," alisema mwanadada huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Tangu nilipokuwa mwanamichezo, sikuwahi kwa kweli kujihisi kuungwa mkono, sikuwahi kuhisi kutambuliwa na wanawake."

Akizungumza katika mkutano wa wanawake mjini Johannesburg, Semenya alisema: "Ninafikiri kwa sababu hawaniwezi ndio maana wananipinga."

Semenya amepinga sheria mpya za mashirikisho ya mchezo wa riadha kuwa yeye na wengine kama yeye wenye kiwango kikubwa cha homoni kutumia dawa za kupunguza ili kuweza kushindana kuanzia mbio za mita 400.

Semenya alikata rufaa mara mbili dhidi ya sheria za Shirikisho la Riadha (IAAF) zinazomzuia kukimbia bila kutumia dawa.

Kuhusu kile kinachoelezwa kutokuungwa mkono na wakimbiaji wenzie wa kike, Semenya alisema: "Mimi ninafanya vizuri. Ukifanya vizuri duniani watu husumbuka na kutokana na unachokifanya."

"Labda mimi ni tatizo kwa sababu nina mafanikio makubwa kupitiliza, hivyo watu wanakuwa kama wanataka kukushughulikia."

"Yeyote atakayenizuia kukimbia anapaswa kuniondoa kwenye mstari wa kukimbia. Sina cha zaidi cha kusema kuhusu suala hili. Ninachoweza kusema ni kwamba nipo kwenye kiwango cha juu."




# Lampard atoa neno kipigo cha Chelsea

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amedai kipigo chao dhidi ya Liverpool kwenye Uefa Super Cup kimechangiwa na timu yake kutopewa muda mzuri wa kujiandaa.

Kocha huyo alisema Liverpool ilikuwa na siku mbili zaidi za kujiandaa na mchezo huo kulinganisha na Chelsea.

Alisema hana furaha kwa kuwa Liverpool ilikuwa na nafasi nzuri kuliko Chelsea katika maandalizi.

"Liverpool ni timu bora, ina wachezaji mahiri, lakini sikuridhishwa na namna mechi yetu ilivyokuwa," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

Hata hivyo, Lampard alidai inaweza ikawa si sababu rasmi iliyochangia kipigo hicho, lakini wapinzani wao walikuwa katika nafasi nzuri ya kushinda.

Chelsea ilifungwa mabao 5-4 kwa penalti baada ya kutoka sare ya 2-2 ndani ya dakika 120 katika fainali hiyo iliyochezwa mjini Instanbul juzi.

Lampard alisema pamoja na kufungwa, lakini ameridhika na kiwango cha wachezaji wake. Kipa wa Liverpool, Adrian aliokoa kiki ya penalti ya Tammy Abraham.

"Hatukucheza vibaya kwa namna walivyopambana, morali na ubora wao. Sitaki kutoa kisingizio, ukweli kulikuwa na tofauti ya maandalizi wenzetu walikuwa na siku mbili zaidi,"alisema Lampard.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK, MESSI, RONALDO NDANI 3-BORA TUZO UEFA

Makocha 80 na waandishi wa habari 55 ndio waliowachagua, mshindi kutangazwa Agosti 29 wakati wa...

**LIVERPOOL, England**

MSHINDI wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Virgil van Dijk, amejiunga na nyota wa Barcelona Lionel Messi na wa Juventus, Cristiano Ronaldo katika orodha ya wachezaji watatu waliopenya kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Uefa.

Van Dijk alikuwa nguzo muhimu katika mafanikio ya Liverpool wakati ikitwaa ubingwa wa Ulaya, akicheza mechi 12 katika safari yao ya kutwaa kombe hilo.

Pamoja na Uefa kumpa heshima hiyo, pia anatarajiwa kuwa mshindani mkubwa kwenye kinyang'anyiro cha tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka 2019 ('Ballon d'Or') kama ilivyo kwa Messi.

Barcelona ilitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa kabla ya kutolewa na Liverpool, lakini Messi bado aliweza kufurahia msimu mzuri wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, alifunga mabao 12ikiwa ni pamoja na mawili dhidi ya Liverpool katika Uwanja wa Camp Nou yakitokana na mechi 10.

Kujumuishwa kwa Ronaldo ni kwa kushangaza hasa ukizingatia Juventus walitolewa na Ajax katika hatua ya robo fainali.

Mshambuliaji huyo wa Ureno alifunga mabao sita katika mechi tisa, lakini hayo yalikuwa madhara yasiyoonekana hasa ukilinganisha na mabao 15 aliyofunga katika mechi 12 alizocheza msimu mmoja kabla.

Orodha hiyo ilichaguliwa na jopo la makocha 80 kutoka kwa klabu zilizoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya na Europa League hatua ya makundi, pamoja na waandishi wa habari 55 kutoka kwa wanachama 55 wa Uefa.

Mmoja kati ya atakayeibuka mshindi atatangazwa Agosti 29, mwaka huu wakati wa hafla ya upangaji wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## KWA UFUPI

**POGBA BADO AIOTA MADRID**
KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba, 26, bado anatamani kuondoka Manchester United na kujiunga na Real Madrid majira haya ya joto. ***(Marca)***

**MAGUIRE ALIVYOIKATAA CITY**
BEKI wa kati wa England, Harry Maguire, 26, alikataa ofa ya pauni 278,000 kwa wiki kutoka kwa Manchester City ili kutoa nafasi ya kutua United. ***(Star)***

**ZIDANE KUMBAKISHA RODRIGUEZ**
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane yupo tayari kumbakisha mshambuliaji Mcolombia, James Rodriguez, 28, ambaye anawindwa na Napoli, ili kupigania namba. ***(Cope Deportes via Mirror)***

**ERIKSEN KAMGOMEA SOLSKJAER**
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alifanya mazungumzo na kiungo wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen kuhusu uwezekano wa kutua Old Trafford, hata hivyo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alitaka kwenda kucheza soka Hispania. ***(Manchester Evening News)***

**SANCHEZ AGEUKA LULU ITALIA**
MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Chile, Alexis Sanchez, 30, anajiandaa kutimkia Italia, wakati huu Juventus, Napoli, AC Milan na Inter Milan zote zikihitaji saini yake. (Mirror)

**DYBALA ATAFUTIWA SOKO JUVE**
Juventus bado inatumai kumuuza mshambuliaji Muargentina Paulo Dybala, 25, kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa - ingawa mabingwa hao wa Italia bado hawajapokea ofa rasmi. ***(Independent)***

**NEYMAR HAKIJAELEWEKA PSG**
MKURUGENZI wa Michezo wa Paris St-Germain, Leonardo amesema mshambuliaji wao Mbrazil Neymar, 27, "amefanya makosa" lakini bado yupo ndani ya mkataba wa "miaka mitatu". ***(RMC - in French)***

**ROJO ANUKIA KUSEPA UNITED**
BEKI wa kati wa Argentina, Marcos Rojo, 29, ambaye alikuwa akiwindwa na Everton majira yote ya joto, inawezekana akaondoka Manchester United kabla ya dirisha la usajili Ulaya kufungwa. ***(Express)***

**LOVREN BADO KIDOGO ROMA**
BEKI wa Liverpool na Croatia, Dejan Lovren, 30, anakaribia kukamilisha uhamisho wake wa kujiunga na miamba ya Serie A, Roma kwa pauni milioni 23. ***(Calcio Mercato via Mirror)***

**UTD ILIVYODUNDA KWA KOULIBALY**
Napoli ilikataa dau la pauni milioni 82 kutoka kwa Manchester United kwa beki Msenegal Kalidou Koulibaly, 28, kabla ya dirisha la usajili la England kufungwa. ***(Corriere dello Sport, via Calciomercato)***

**BUTLAND KUMSHAWISHI SOUTHGATE**
KIPA wa Stoke City na England, Jack Butland, 26, atahitaji kwenda kucheza soka nje ili kulazimisha njia ya kuitwa katika kikosi cha Kocha wa England, Gareth Southgate kuelekea Euro 2020. ***(Mail)***

**FLAMENGO YAMPOTEZEA BALOTELLI**
KLABU ya Flamengo ya Brazil imeweka kando mchakato wa kwenda kumsajili mshambuliaji huru, Mario Balotelli, 29, kutokana na dau la pauni milioni nne analohitaji mchezaji huyo katika mkataba atakaosaini. ***(Mail)***

**LOZANO, NAPOLI WAKUBALIANA**
Napoli imekubali dili la kumsajili winga wa Mexico, Hirving Lozano, 23, kutoka kwa PSV Eindhoven ya Uholanzi. ***(Voetbal International - in Dutch)***

## HABARI MICHEZO

# KMC YAJA NA 'TOGETHER WE CAN' KUIUA AS KIGALI

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikiendelea kujiwinda na mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali ya Rwanda, uongozi wa KMC FC, umekuja na kaulimbiu ya "Together We Can" ikiwa ni njia muhususi ya kuhamasisha mashabiki kujitokeza kwa uwingi uwanjani kuishangilia.

KMC FC ikiwa ugenini Rwanda, ililazimisha sare tasa, hivyo inahitaji ushindi wowote katika mechi ya marudiano itakayopigwa Uwanja wa Taifa kati ya Agosti 23-25, mwaka huu ili kusonga mbele.

Kaulimbiu hiyo ya KMC karibu ifanane na ile ya Simba ya msimu uliopita ya "Yes We Can" wakati ilipofika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kama ambavyo, Msemaji wa Simba, Haji Manara, alivyoonyesha ubunifu wake kwa kuja na kaulimbiu hiyo ya "Yes We Can", ndivyo ambavyo Ofisa Habari wa KMC, Anwari Binde naye ameitambulisha kaulimbiu hiyo ya "Together We Can".

"Tunatambua itakuwa mechi ngumu, timu yetu ipo katika maandalizi mazito kuelekea mchezo huo dhidi ya AS Kigali, tumeamua kuja na kaulimbiu ya "Together We Can" lengo likiwa ni kuongeza hamasa na nguvu kwa mashabiki kuelekea kwenye mchezo wetu," alisema.

Aidha, aliwaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi kuipa sapoti timu yao huku akiahidi kikosi chao kutoa burudani ya kuvutia.

Mshindi katika mechi hiyo atakutana na mshindi kati ya Proline FC ya Uganda anapo-




Wachezaji wa Azam wakipongezana baada ya kupachika moja kati ya mabao nane waliyofunga dhidi ya Namungo FC katika ushindi wa 8-1 walioupata kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Chamazi juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mbio za mbuzi kulipia wanafunzi

**Na Mary Geofrey**

KLABU ya Rotary Oysterbay, imeandaa mashindano ya mbio za mbuzi, kwa ajili ya kuchangisha fedha za kusaidia kusomesha wanafunzi wa elimu ya juu takribani 60 wasiyo na uwezo.

Kupitia mashindano kama hayo yaliyofanyika mwaka jana, jumla ya wanafunzi 42 wa vyuo vikuu mbalimbali nchini, walipata ufadhili wa masomo.

Rais wa Rotary Dar es Salaam, Amish Shah, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, alisema kwa mwaka huu mashindano hayo yatafanyika Septemba 29.

**Alisema fedha watakazo pata katika mashindano hayo wanatarajia kuz ielekeza katika ufadhili wa masomo kwa wa nafunzi wa vyuo vikuu ambao hawana uwezo wa kulipa ada.**

"Tunawakaribisha Watanzania katika mashindano haya ya kufurahisha ambayo tumeona washiriki watafurahi na kusaidia kuchangia fedha za kusaidia wahitaji ndani ya jamii," alisema Shah.

Alisema wanafunzi waliowafadhili masomo mwaka jana asilimia 41 kati yao ni wasichana na wanasomea fani mbalimbali zikiwamo za uhandisi na udaktari katika vyuo tofauti nchini.

# Sauti Sol kupamba 'Rhumba Festival' 2019

**Na Faustine Feliciane**

KUNDI la muziki wa Rhumba kutoka Kenya la Sauti Sol, linatarajia kutoa burudani kwenye tamasha maalum la muziki huo lililopewa jina la 'Rhumba Festival' litakalofanyika jijini Dar es Salaam Agosti 30, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya TIST International Limited waandaaji wa tamasha hilo, George Kyatika, alisema wamekuja na tamasha hilo litakalokuwa likifanyika kila mwaka hapa nchini.

Alisema muziki wa Rhumba ni aina tofauti ya muziki ambayo haupotezi ladha yake, hivyo anaamini wapenzi wa muziki huo watapata burudani ya kutosha.

"Tumejipanga kuhakikisha tamasha hili linafanikiwa kwa asilimia kubwa na kuwapa wapenzi wa muziki huu burudani ya kutosha kutoka kwa wanamuziki hawa wa Kenya na wengine kutoka hapa nyumbani," alisema Kyatika.

Aidha, alisema kampuni hiyo kwa sasa ipo kwenye mazungumzo ya mwisho na baadhi ya wasanii wakubwa wa hapa nchini kuweza kushiriki kwenye tamasha ilo litakalofanyika Ukumbi wa Next Door, Masaki jijini Dar es Salaam.

"Baada ya mkutano huu tutakuwa tukiwatangaza wasanii wengine wa hapa nyumbani ambao watapanda jukwaa moja na Sauti Sol, wapo wasanii wakubwa watashiriki," aliongeza kusema.

"Rhumba ni muziki wa watu wastaarabu ambao wanacheza bila kutoka jasho au kutumia nguvu, una vionjo vya Kiafrika na unapendwa sana, kwa kuona hivyo sisi TIST tumeamua kuwa na tamasha la muziki huu la kila mwaka na kwa kuanzia ndio tunazindua na Sauti Sol, mashabiki wajitokeze kwa wingi kufurahia muziki huu wa 'watu wazima'," alisema.

Kwa upande wake Meneja Matukio wa kampuni hiyo, Neema Mbuya, alisema kuwa maandalizi yote yanaendelea vizuri na wapo kwenye hatua za mwisho kabla ya kufanyika kwa tamasha hilo.

"Ulinzi utakuwa wakutosha na kila kitu muhimu kitapatikana siku ya tamasha, tunawashauri wadau wa muziki huu kununua tiketi mapema ambazo zitapatikana Sh. 50,000 na 100,000.

# FRAT: Wadhamini wametukwamisha

**Na Shufaa Lyimo**

MKUTANO Mkuu wa Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT) ambao ulipangwa kufanyika kesho, hautafanyika kutokana na kukosekana kwa wadhamini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa FRAT, Joseph Mapunda, alisema mkutano huo hautafanyika mpaka hapo tarehe itakapopangwa upya.

"Tumeahirisha mkutano wetu ambao ulikuwa ufanyike mwezi huu, kuna sababu zimesababisha kushindwa kufanya mkutano huo," alisema Mapunda.

Aliongeza kuwa kwa sasa hawana katibu mkuu na kufafanua kuwa nafasi yake ipo wazi baada ya aliyekuwa amekalia kiti hicho, Odeni Mbaga kufungiwa.

"Nafasi ya katibu ipo wazi mpaka sasa, bado hatujapata katibu mkuu," alisema mwenyekiti huyo.

Michezo
Jumamosi Agosti 17, 2019
Nipashe



## Van Dijk, Messi, Ronaldo ndani 3-bora

HABARI UK 30



Etienne Ndayiragije

Aussems

# SIMBA, AZAM NA DK. 90 ZA JASHO

●●● Makocha watambiana huku kila mmoja akitaja majeruhi wake, TFF yaanika waamuzi, Ajibu sasa...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba na wafalme wa Kombe la Shirisho la Soka nchini (FA Cup), Azam FC, wakitarajiwa kushuka dimbani leo tayari kwa mechi ya Ngao ya Jamii maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa 2019/20, mchezo huo unatarajiwa kuwa wa mchakamchaka kwa dakika zote 90, imeelezwa.

Timu hizo zitashuka katika Uwanja wa Taifa leo kila moja ikipania kuanza msimu na taji, lakini pia zikiutumia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi ya mechi zao za kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba inawania kutwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo na mara ya saba kwa ujumla wake, wakati Azam ipania kulibeba kwa mara ya pili.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuelekea mechi hiyo, makocha wa timu hizo kila mmoja alionyesha kupania kuanza msimu kwa kombe hilo ambalo hukutanisha bingwa mtetezi wa Ligi Kuu Bara na yule wa Kombe la FA.

Kocha wa Makipa wa Simba, Muharami Mohamed, alisema: "Tumejiandaa vizuri kwa mchezo wa Ngao ya Jamii ili tuchukue kombe ambalo hata mwaka jana tulichukua. Tuna majeruhi watatu (Ibrahim) Ajibu, (Aishi) Manula na Wilker Da Silva na waliobaki wote wapo tayari kwa mchezo."

Aidha, aliwataka mashabiki wao kujitokeza kwa wingi uwanjani leo kuona kazi inayofanywa na vijana wao kwa kuwa wamekiandaa kikosi chao kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuweka kambi nzuri nje ya nchi.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo ambao utakuwa na ushindani mkubwa tunaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kesho (leo),"alisema Mwalami.

Kauli hiyo ya Muharami haipishani na ile ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Patrick Aussems aliyoitoa katikati ya wiki akisema: "Tunataka kuanza na kombe na mipango yote ni dhidi ya Azam na baada ya hapo tutageukia mechi ya marudiano Ligi ya Mabingwa dhidi ya UD Songo."

Kwa upande wa Azam FC, licha ya kueleza kuwa mchezo wa leo watawakosa nyota wao wawili Mudathir Yahya na Aggrey Moris ambao ni majeruhi, walisema hilo haliwezi kuwa sababu ya kushindwa kufurukuta.

Kocha msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche alisema, maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika kwa asilimia 95, na kudai kila mchezaji ana morali ya ushindi.

"Wachezaji wote wapo salama isipokuwa hao wawili mchezo wa kesho tunaupa umuhimu mkubwa ukizingatia tunajiandaa na mechi yetu ya marudio ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Waethiopia (Fasil Kenema)," alisema Cheche.

Naye Msemaji wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Cliford Ndimbo, aliwataja waamuzi watakaochezesha mchezo huo kuwa ni Mwamuzi wa Kati Elly Sassi kutoka Dar es Salaam akisaidiwa na Frank John Komba, mwamuzi msaidizi namba moja (Line 1) wa Dar, wakati mwamuzi msaidizi namba mbili (Line 2) atakuwa Mohamed Mkono kutoka Tanga.

Mwamuzi wa akiba (Forth Official) atakuwa Ferdinand Chacha kutoka Mwanza huku Jonesia Rukiyaa kutoka Kagera akiwa msaidizi upande wa goli la kwanza na Martin Saanya wa Morogoro atakuwa msaidizi upande wa goli namba mbili.

# Matola aendelea kumtesa Zahera

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuitesa Yanga msimu uliopita wakati akiinoa Lipuli FC ya Iringa, Kocha wa Polisi Tanzania, Seleman Matola, ameendeleza rekodi yake ya kukifunga kikosi hicho kinachonolewa na Mwinyi Zahera baada ya jana kukichapa mabao 2-0 katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Msimu uliopita katika raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara, Yanga iliichapa Lipuli bao 1-0 Uwanja wa Taifa kabla ya vijana hao waliokuwa wakinolewa na Matola kulipa kisasi kwa ushindi kama huo na kisha kuitoa katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho (FA Cup) kwa kuichapa 2-0.

Katika mchezo wa jana ambao Yanga iliutumia kama maandalizi ya mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana huku Polisi Tanzania ikijiandaa na Ligi Kuu msimu wa 2019/20, ilipata bao lao mapema tu dakika ya sita kwa mkwaju wa penalti, baada ya beki wa Yanga kuunawa kwenye eneo la hatari katika harakati za kutaka kuokoa.

Alikuwa ni straika wa zamani wa Majimaji na Simba, akapelekwa kwa mkopo AFC Leopards ya Kenya, kabla ya kurejea nchini na kujiunga na Polisi Tanzania kwa mkopo, Marcel Kaheza, aliyeizamisha nyavuni na kumuacha kipa Ramadhani Kabwili akiruka upande wa kushoto na mpira kuingia kulia kwake, huku bao la pili likizamishwa kimyani na straika wa zamani wa Majimaji, Mbeya City na Mwadui FC, Ditram Nchimbi katika dakika ya 74.

Yanga itarudi tena dimbani kesho Jumapili katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya AFC Leopards ya Kenya.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042